CHUO CHA BIBLIA

NDOA NA JAMII
(Sehemu Ya Kwanza)

KITABU CHA SITA

Vipindo Saba Vinavyounganisha Ndoa

1. KIROHO
(Msingi)

2. MAWASILIANO
(Chombo)

3. UTANGAMANO
(Ishara)

4. UPENDO
(Uwezo)

5. UFAHAMU
(Kukua)

7. KIROHO
(Msingi)

6. NGONO/ KUJAMIIANA
(Udhihirisho wa Furaha)

Sura ya 1

Sheria Ya Ndoa Na Jamii

Miaka mingi iliyopita huko Marekani, mtu mmoja alikuwa na matatizo ya kimitambo na gari lake ambalo lilikuwa limezeeka, kwa hivyo aliamua kuliegesha kando mwa barabara. Ikawa muungwana mwingine aliyekuwa amevaa mavazi nadhifu kabisa, ambaye pia alikuwa

akiliendesha gari lake kwenye njia ile ile, akalilisimamisha kando karibu na lile gari lililokuwa limeharibika ili kumsaidia mwenzake mwenye gari kuu kuu. Akashuka toka kwenye gari lake na kufungua mbele kwenye sehemu ya mitambo ya lile gari lililokuwa limeharibika. Gari hilo lilikuwa aina ya *Ford*, muundo wa gari ambao ni maarufu sana huko Marekani. Muungwana huyo aliyekuwa amejivika nadhifu sana alianza kurekebisha mtambo wa lile gari na punde likawa tayari. Yule mtu mwenye gari hilo alimwuliza yule muungwana, *'unawezaje kulifahamu hivyo gari hili la Ford?' Huyu muungwana akamjibu, 'Mimi ndiye Henry Ford. Mimi ndiye niliyeunda na kulijenga gari hili, nami ndiye mwenye kiwanda kinachojenga magari haya.'*

Jinsi tunavyoweza kumtarajia *Henry Ford* kutueleza jinsi ya kulirekebisha mojawapo ya magari yake, pia tunaweza kumtarajia Mungu kutueleza jinsi ya kurekebisha ndoa, kwa kuwa Yeye ndiye aliyeiunda. Msingi wa kanuni hizi za ndoa na jamii uko katika Maandiko. Dhana yake yaengemea katika kweli kwamba Mungu ndiye mwenye kuunda ndoa na jamii, Mungu ndiye awezaye kutueleza jinsi ya kurekebisha ndoa iliyovunjika. Mungu pia anaweza kutueleza maana na nia ya ndoa, na hatimaye nakala Yake kwa ndoa na jamii.

Yesu Alifunza Nini Kuhusu Ndoa Na Jamii?

Sisi ambao tu wanafunzi wake Yesu Kristo twahitajika kulianza kila somo kwa kuuliza swali hili, 'Yesu alifunza nini kuhusu ndoa na jamii? Wakati viongozi wa dini walipomwuliza Yesu kuhusu ndoa na talaka, Yeye aliwajibu kwa swali lingine: *'Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke?'* **(Mathayo 19:4).** Yesu alikuwa akisema kuwa, 'ikiwa unataka kufahamu kufahamu ndoa jinsi ilivyo, ni lazima urudi hadi mwanzo na kusoma ndoa jinsi Mungu alivyokusudia iwe.'

Nakala Ya Mungu Kuhusu Ndoa

'Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; . . . Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi na kuitiisha' ***(Mwanzo 1:26-28).***

Kote katika maelezo ya uumbaji, Mungu anatazama vyote alivyoumba na kusema, *'Ni chema sena.'* Lakini unapofikia sura ya 2, unakumbana na maneno haya, *'Si Vema.'* Ni kipi kilichokuwa si vema? Ilikuwa si vema huyo mtu awe peke yake. *'Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume. Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.'* ***(Mwanzo 2:21-24).***

Mungu alionelea mwamamume akiwa peke yake kuwa si mkamilifu. Neno la Kiebrania katika fungu hili la maneno haya inadokeza kuwa, *'Nitamfanyia yeye mkamilishaji wake.'* Hii ndiyo maana ya msaidizi au *'Msaidizi wa kumfaa,'* katika lugha ya Kiebrania - 'Mkamilishaji.' Tokea mwanzoni Mungu alitupatia maelezo ya ndoa na jamii. Mwanamume si mkamilifu bila mwanamke. Mwanamke ameumbwa ili kumkamilisha mwanamume.

Maelezo kuhusu uumbaji yamerudiwa tena katika sura ya pili, na kwa mara ya tatu katika **Mwanzo 5:1-2,** mkazo ukitiliwa juu ya Mungu kumuumba binadamu mwanamume na mwanamke. Hakikisha kwamba umelitilia jambo hilo maanani, kwamba katika **Mwanzo 5**, Mungu hawaiti 'mume na mke wa Adamu,' bali 'Adamu.' Na kuwa jina ' Adamu' linamaanisha, 'mwanadamu,' hii inatufundisha kwamba mwanamume na mwanamke wakishikamana pamoja katika ndoa takatifu huwa mwanadamu mmoja mkamilifu. Hii ni njia nyingine ya kusema kwamba hawa wawili wameumbwa kuwa kitu kimoja.

Watu, Washirika Na Wazazi

Kile tunachokiona hadi hapa katika Maandiko ni sheria ya maisha. Tunaweza kuitaja kama 'Sheria Ya Ndoa Na Jamii.' ili mpango huu ufaulu, ni lazima Mungu awe na wazazi wawili wakamilifu. Na ili kuwepo na ushirika mkamilifu, ni lazima wawe watu wakamilifu.

Wakati alipomuumba Adamu na Hawa, ushirika ambao Mungu alitayarisha haukuwa wa kupe wawili wanyonyaji waliojaribu kunyonya uhai wa kila mmoja wao. Wala mfumo huo haukuwa kati yake binadamu na kupe, pale ambapo mtu mmoja anamnyonya mwenzake uhai wake wote. Mpangilio ulikuwa - na ni - kwamba watu wawili wakamimilifu ambao wanayajenga maisha yao wenyewe kwa pamoja jinsi Mungu alivyokusudia wakati alipomuumba mwanamume na mwanamke. Kanuni hii ni ya kweli hata siku ya leo jinsi ilivyokuwa wakati wa uumbaji.

Hata hivyo, nakala hii imekubwa na shutuma kali sana siku ya leo. Kwa mfano, nakala inayokubalika kati ya mwanamume na mwanamke siku ya leo inasema kwamba mwanamke ni sharti athibitishe usawa wake na mwanamume kwa kutenda yote ambayo mwanamume hutenda. Wazo ni kwamba ikiwa yeye hawezi kuwa na wajibu sawa na mwanamume, basi yeye hana thamani sawa naye.

Wanaume hujigamba kuwa dume ilhali wanawake nao hutangaza ukuu wao kana kwamba uhusiano kati ya mume na mke ulikuwa sawa. Kulingana na nakala ya Biblia, uhusiano wa mke-mume ni wa wote/ na wa umoja. Ikiwa hawa wawili wangelikuwa wamefanana kabisa, basi mmoja wao hangehitajika. Mungu kwa kusudia alituumba kwa njia ya kipekee- mwanamke na mwanaume ili tuweze kujumlishana moja kwa mwingine. Desturi na tamaduni zinatisha kuangamiza tofauti kati ya utu wa kike na wa kiume kwa kuzifanya jukumu pamoja na wajibu wa wanaume na wanawake kusawazishwa. Lakini kuna mgawanyiko mzuri na wajibu wa ajabu Mungu alivyoumba mwanamume na mwanamke.

Njia moja ya kuelezea amri hii kuu ya ndoa na jamii ni kupitia mchoro wa pembe tatu wenye kugawanyika sehemu tatu. Katika sehemu ya chini ya msingi wake, andika 'watu' ilhali katikati andika 'ushirika,' na hatimaye juu kabisa andika 'wazazi.'

Wazazi

Washirika

Watu

Ili kujenga haram au pembe tatu, hauwezi kuanza ujenzi wako kuanzia juu. Na kwa njia ile ile, sio mpango wake Mungu kuanza ujenzi wa jamii na wazazi wawili ambao hawana ushirika ulio changuo Lake. Zaidi ya hayo, sio mpango wake Mungu kuwa na sehemu ya katikati katika pembe tatu bila sehemu ya chini ya tatu. Msingi wa ushirika ambao huwafanya wazazi bora ni watu wawili wakamilifu. Sehemu ya chini katika jengo hili la pembe tatu ni msingi. Vivyo hivyo, sehemu muhimu ya ndoa ni watu wawili ambao huunda ndoa ile.

Mahali Pa Kuanzia

Kuna shida nne katika kila ndoa. Kati ya ndoa yake Yohana na Mariamu, shida ya kwanza ni Yohana. Shida ya pili ni Mariamu. Shida ya tatu ni Yohana pamoja na Mariamu na mambo yao ya usawa. Wana wa Yohana na Mariamu ndio shida la nne katika ndoa yao.

Ikiwa Yohana ana shida hamsini, naye Mariamu vile vile ana shida hamsini, ndoa yao ina shida mia moja kabla hawajaongezea shida zao zote za kibinafsi kwa pamoja. Ikiwa Yohana ataamua kwamba anataka kushughulikia ndoa yake, anahitajika kuanzia na shida ya kwanza - Yeye binafsi. Naye Mariamu anahitajika ashughulikie kwanza shida ya pili - Yeye binafsi. Ikiwa

wewe hauwezi kukiri kweli kwamba u sehemu ya shida, basi hakuna mshauri wa ndoa katika ulimwengu huu ambaye anaweza kuiokoa ndoa yako. Lakini ikiwa utashuluhisha shida katika maisha yako, utakuwa umeshuluhisha shida nyingi sana katika ushirika huo.

Hebu nishiriki nawe katika hadithi ambayo inaelezea jambo hili: mtu mmoja alikwenda kwa daktari wa mambo ya akili na hisia akiwa na mboga ya Saladi *(Lettuce)* mkononi pamoja na mayai matatu juu kichwa chake, sawa na kipande cha nyama ya kondoo kwenye kila sikio lake. Daktari alimkaribisha kwake aketi kwenye kiti. Huyu mtu aliketi kwa uangalifu sana ili kwamba yale mayai yasianguke chini kutoka kwenye kichwa chake. Yule Daktari akamwuliza, 'Je! *Ungependa kulijadilia jambo hili?*' Naye akamjibu, '*Naam, Daktari, ningelipenda kuzungumza nawe kuhusu ndugu yangu. Naam, ndugu yangu, kwa hakika ni mwenye matatizo mengi mno.'*

Wachungaji na washauri wengi wa maswala ya ndoa hukutana na watu wa aina hiyo kila siku, watu ambao hawawezi kukiri kwamba wao ni sehemu ya shida. Jinsi vile Yesu alivyosema, *'Wewe ni mwenye gogo au kisiki ndani ya jicho lako, lakini unazunguka kote ukitafuta vibanzi machoni mwao watu wengine.'* **(fafanusi la Mathayo 7:3,).** Watu wenye kuwakosoa wale wengine ni stadi katika yale yaliyo mabaya kwa wenzao hasa nyumbani mwao na katika ndoa. Wao huwalaumu watu wengine na hawaamini kuwa wanaweza kuwa sehemu ya shida hata wakati ni dhahiri kwa kila mmoja kwamba wao ndio sehemu kuu katika shida ile.

Ushauri mkuu duniani wa ndoa unapatikana katika Biblia. Katika kitabu hiki, tutazama baadhi ya mashauri yanayopatikana katika Biblia. Tunapofanya hivyo, tutagundua baadhi ya mitindo na kanuni. Mojawapo ya mitindo ni huu: kila mara Biblia inapozungumzia kuhusu ndoa huwa inawaunganisha washirika wawili wa ndoa kuwa mtu mmoja. Kisha huzungumzia wajibu wake mume. Inapofanya hivyo, humweleza mwanamume wajibu wake katika ndoa. Inapomzungumzia mwanamke pia , Biblia humwongoza katika wajibu wake katika ndoa.

Kwa mfano, waraka wa kwanza wa Petro sura ya tatu unaanza kwa kuwazungumzia wanawake, hasa wanawake ambao waume zao hawatii neno. Katika aya sita sinazofuatia, Petro hasemi jambo kuhusu waume. Badala yake, anawaamuru wanawake kuhusu maswala bali bali kama usafi, mavazi, na kunyenyekea. Anawaambia wanawake kuanza na shida nambari mbili. Wanapaswa kumwuliza Mungu kuwafanya kila kitu anachotaka wao wawe na kufanya katika ndoa yao.

Baadaye, Petro anawazungumzia waume kuhusu shida nambari moja. Biblia huzungumzia mambo yale kwa njia halisi na ya utendaji. Maandiko pia huwazungumzia watoto kuhusu wajibu wao kwa wazazi. Biblia huwa hakika wakati itendapo hivyo kwa sababu; njia ile ambayo unaweza kutenda jambo lo lote ni kwa mtu yule ambaye unawajibika kwake - wewe binafsi.

Inawachukua baadhi ya watu walio katika ndoa wakati mrefu kujifunza hili, lakini katika jumuiko la mwisho, utajifunza kisha baadaye kusema, *'Siwezi kutenda lo lote kumhusu mwenzi wangu.'* Kwa hakika hauwezi kutenda cho chote. Katika kiti cha hukumu, wewe hautawajibika kuhusu mwenzi wako mbele Zake Mungu. Wewe hautawajibika kujibu lo lote mbele zake Mungu kwa niaba ya mwenzio. Badala yake, utawajibika kwake mtu mmoja ambaye wewe kwa hakika unawajibika kwake. Utawajibika kwa ajili yako binafsi. Wewe utakuwa mwenye hekima ikiwa utaanza kuwajibika sasa kwa njia ya kuwa na uwajibikaji kwa mtu yule uwezaye kumwongoza katika ndoa.

Mara kwa mara katika mashauri ya ndoa, mchungaji au mshauri hawezi kukutana na mke pamoja na mume kwa kuwa yeye hufanyika kama refa msimamizi wa pigano hilo. Atakuwa mwenye busara ikiwa atakutana na kila mmoja wao binafsi. Baada ya kumsaidia kila mmoja wao kibinafsi na kushughulikia shida zake, sasa anaweza kusongea katika ushirika wao pamoja na mambo ya usawa. Ikiwa hawa watu sio waaminifu ambao wana uhusiano wa kibinafsi naye Yesu Kristo, jukumu kuu lake mchungaji huyu litakuwa kuwaongoza katika wokovu na uhusiano naye Mungu kumpitia Kristo. Ushauri wa ndoa unaweza kuwa chombo chenye mazao kwake mshauri wa kiroho au mchungaji.

Mume mmoja aliambiwa hivi na mchungaji wake, *'Siyo mkataba wa hamsini kwa hamsini; wala si watu wawili mia moja kwa mia moja kwa kila mmoja wao. Ndoa ni watu wawili waliojitolea kwake Mungu asilimia Mia moja kamili;'* Yule mume alikwenda nyumbani kwake na kumwambia mkewe, *'Mchungaji alisema ndoa ni mia moja kamili. Mimi ndiye asilimia mia moja nawe hauna.'* Watu wengine wanakubwa na wakati mgumu kutambua ukweli mzito kwamba 'Watu' ndio msingi wa jengo la ndoa. Hapa ndipo shida za ndoa huanza na suluhisho za shida hizo ni lazima zianzie hapo. Wanapoukubali ukweli huo, ni lazima pia watambue kwamba mtu anayepaswa kuanza ni yule ambaye anaweza kutenda jambo fulani kuhusu shida yao - ni lazima waanze kwao binafsi.

Maana Ya Ndoa Kwa Mungu

Kama ulianza katika somo hili la ndoa na jamii ukiuliza, 'Ni kipi kipo kwa ajili yangu katika ndoa hii?' Jibu ni kwamba yapo mambo mengi sana ndani kwa ajili yako. Jambo hilo ni nyumba yenye furaha. Lakini ikiwa kweli unataka kupata mtazamo wa Kibiblia kuhusu somo hili la ndoa na jamii, basi unahitajika kuuliza swali hili, 'ni kipi kipo kwa ajili yake Mungu katika ndoa?' Ndoa inamaanisha nini kwake? Mbona alianzisha ndoa? Mbona alituumba sisi wake kwa waume? Jibu ni kwamba Mungu alitaka kuijaza dunia kwa watu wema.

Zaburi 128 ni mojawapo ya maelezo sahihi na muhimu kuhusu mpango wake Mungu. *'Heri kila mtu amchaye Bwana, Aendaye katika njia yake. Taabu ya mikono yako hakika utaila; Utakuwa heri na kwako kwema.'* **(1-2).** Watu wengi hupenda kuweka alama ya kikomo baada ya neno la tatu la msitari wa 1: 'Heri kila mtu.' Katika siku ya leo, watu wengi wahubiri elimu ya Kujumlishwa *(Universalism)* ambayo sehemu yake husema Mungu ni mwenye upendo, watu wote wamebarikiwa. Lakini Maandiko anafundisha jambo hilo. Hii ni moja wapo ya Zaburi zake 'Mwenye heri', somo lilio katika kitabu cha Zaburi. Zaburi hizi zatufundisha kwamba baraka zake mwenye heri sio ajali wala tukio la bahati. Ni matokeo ya imani na utiifu kwake Mungu.

Mkazo wa Zaburi hii yake mwenye heri ni kutuonyesha jinsi ambavyo Mungu humtumia na jinsi mwenye heri ni mwenyewe utangamana na mtindo na mpango wake Mungu. Mwimbaji wa Zaburi aendelea kusema, *'Mkeo atakuwa kama mzabibu uzaao, vyumbani mwa nyumba yako. Wanao kama miche ya mizeituni wakiizunguka meza yako. . . Bwana akubariki toka Sayuni; Uone uheri wa Yerusalemu siku zote za maisha yako; Naam, ukawaone wana wa wanao. Amani ikae na Israeli* **(128:3, 5-6).**

Haya ni maelezo kuhusu jinsi Mungu hutenda kazi ulimwenguni. Yeye hutenda kazi kupitia sheria ya ndoa na jamii. Yeye humtafuta mtu ambaye atamwamini na kutembea katika njia Zake, na kumbariki yule mtu. Anapomleta mwanamke katika maisha ya yule mtu na kumkamilisha, Mungu humfanya kuwa baba. Na kutokana na hawa watu wawili kufanyika ushirika, wao huzaa jamii. Hawa watoto huwa pamoja nao kwa muda wa takribani miaka ishirini, wakipewa malezi na kutayarisha kukumbana na maisha. Hii hufanyika sehemu ya Sayuni (Jamii ya kiroho katika Agano la Kale), ili kuugusa mji wao (Yerusalemu), taifa la (Israeli), na hatimaye ulimwengu.

Katika Agano la Kale, neno Sayuni ni sawa na dhana iliyopo katika Agano la Kale kuhusu Kanisa. Je! Mungu huitenda kazi yake katika ulimwengu kwa njia ipi? Wafuasi wake Kristo hufikiri kwamba kwa wakati mwingi, yeye huitenda kazi yake kupitia Kanisa. Mungu na Kristo hutenda kazi kupitia Kanisa, lakini Kanisa ni vipengele vya jamii. Kipengele kidogo kabisa katika ulimwengu ni jamii. Mungu hutumia kipengele cha jamii ili kugusa Sayuni (Kanisa). Wakati vipengele hivi vinapokusanyika katika jamii ya kiroho, wao husawishi mji na taifa na hatimaye ulimwengu. Na ikiwa mambo hayako sawa ulimwenguni, na ikiwa hayako sawa katika taifa na jiji, basi ni wapi unapata shida na suluhisho? **(Zaburi 68:6).**

Miaka kadhaa iliyopita, jarida moja lilichapisha toleo moja maalumu kwa ajili ya shida za watoto na uhalifu. Wengi wa waandishi wenye ujuzi mwingi waliweza kugusia baadhi ya uwezekano. Je! Ilikuwa ni kosa la Serikali? Je! Ilikuwa ni kosa la elimu? Au ni shida la mila na desturi? Baadhi ya waandishi waligusia Makanisa, Masinagogi, na Misikiti. Baadhi ya mashirika haya inawezekana kwamba hayakutenda yale waliyohitajika kutenda. Lakini hatimaye,

wataalamu wa saikolojia na majaji wanaoshungulikia mahakama za watoto pamoja na wafanyi kazi ya maswala ya kijamii waliafikiana kwamba: msingi au chanzo cha shida za watoto na uhalifu ni jamii.

Wajibu Wa Mwanamume

Kulingana na sheria ya ndoa na jamii katika Biblia, jukumu huanzia na mume. Tunapochunguza shida za ndoa na jamii leo, naamini kuwa shida kuu ni wanaume ambao hawakubalii wajibu wao jinsi Mungu alivyonuia mwanamume awe kichwa cha nyumba yake - kuhani wa kiroho nyumbani mwake. Kulingana na **Zaburi 128,** baraka yake Mungu katika ulimwengu huu huanza wakati mtu amemwamini na kutembea katika njia zake. Wakati mtu anapoamini Mungu na anatembea katika njia Zake, Mungu ana msingi ambao anaweza kujenga jengo Lake la kijamii lenye pembe tatu. Yeye anaweza kuiweka sheria ya ndoa na jamii mahali pale kwa kuwa Amempata mtu aliyebarikiwa. Hapa Mungu anaweza kuunganisha mtu huyu aliyebarikiwa pamoja na mwanamke aliyebarikiwa nao wanaweza kuwa na watoto waliobarikiwa. Na sasa, Mungu anaweza kuibariki ile nyumba, Kanisa, jiji, taifa na ulimwengu. Yote huanza na mtu aliyebarikiwa.

Kuvunjika kwa jamii na ndoa ambako kumekita mzizi siku hizi, kumewaacha watu wengi wa makamu bila watuzi wakuiga. Kuna watu kadhaa ambao wamewataka wachungaji kuwa baba wao kwa kuwa wao hawakuwa na baba mzazi. Mtu fulani ambaye alikuwa ameoa kwa miaka kadhaa alimwendea mchungaji na kumwambia, *'Mimi sitaki kuwa na watoto hadi wakati nitafahamu jinsi ya kuwa baba mzazi. Je! Wewe utafanyika kuwa baba yangu kwa muda kidogo?'*

Watu wawili walioposana walimwendea mchungaji kwa ushauri kabla ya ndoa na kuwaambia, *'Sisi tuna hofu kubwa sana kuhusu kuwa na ndoa iliyofanikiwa. Ndoa nyingi sana zimemalizikia katika talaka, nasi hatujawahi kuiona ndoa njema. Wazazi wetu waliachana, nasi hatufahamu ndoa na jamii yao Wakristo inakaa vipi. Je! Sisi tunaweza kuwa na uhakika wa aina gani kuwa tunaweza kuwa na ndoa na jamii yenye furaha?'*

Hivyo basi, ni jinsi gani uwezavyo kuijenga na kuituza nyumba yenye furaha? Sulemani, mtu mwenye hekima kuu kuwahi kuishi, anatumia mojawapo ya maneno apendao wakati anapoiandika **Zaburi ya 127**, *'Bwana asipoijenga nyumba Waijengao wafanya kazi bure. Bwana asipoulinda mji Yeye aulindaye akesha bure. Kazi yenu ni bure, mnaoamka mapema, Na kukawia kwenda kulala, Na kula chakula cha taabu; Yeye humpa mpenzi wake usingizi.'*

Mistari hii miwili ni jumla ya hadithi ya maisha yake Sulemani, au wosia wa maneno yenye hekima ya maisha yake. Zaburi hii fupi ni muhtasari wa ujumbe wake mkuu uitwao 'mhubiri.' Neno alipendao mno katika muhtasari wa aya hizi mbili ni 'ubatili mtupu.'

Sulemani alikuwa kielelezo kikuu cha zamani kuhusu mfanyi kazi bila kuchoka, ilhali anatueleza hapa kwamba inawezekana kuifanya kazi kwa ubatili mtupu. Yawezekana kwamba alihofia mambo mengi, lakini hapa anatuambia ni ubatili kuamka mapema, kwenda kitandani umechelewa na kula chakula cha taabu. Yeye pia anatuambia kwamba inawezekana kujenga kwa ubatili. Sulemani alikuwa mjenzi mkuu. Yeye hakulijenga Hekalu tu bali pia alijenga miji na

bustani pamoja na makao ya farasi. Wakati mmoja alijenga kundi la merikebu ili kwenda kumwamkua malkia pekee tu. Hapakuwa na mwisho katika ujenzi wake.

Yawezekana kuhofia bure kwa maana yanaweza kuwa mambo mabaya. Yawezekana pia kuifanya kazi ya bure kwa kuwa haina maana. Inawezekana kujenga bure kwa kuwa waufanya ujenzi usio faa.

Kisha Sulemani anageukia hoja ya watoto. Je! Maelezo haya yanahusika kwa njia gani na watoto? Kila kitu. Sulemani alitambua kwamba aliufanya ujenzi wa kila kitu isipokuwa maisha ya wanawe. Na hapa, mfalme huyo mwenye hekima anasema haya, *'Tazama, wana ndio urithi wa Bwana, Uzao wa tumbo ni thawabu. Kama mishale mkononi mwa shujaa, Ndivyo walivyo wana wa ujanani. Heri mtu yule Aliyelijaza podo lake hivyo. Naam, hawataona aibu Wanaposema na adui langoni'* **(3-5).**

Zaburi hii ni kinyume cha sheria ya ndoa na jamii. Sulemani asema hivi, *'Usilitende lile nililolitenda kwa kuwa mimi nilifanya kazi ya bure na kuhofia bure.* Kile unachohitaji hasa ni *kujishughulisha mwenyewe na watoto wako.'* Anamalizia Zaburi hii kwa fumbo lenye uzito mkuu ambapo anatuambia kwamba wazazi ni kama upinde kwa watoto wao, jinsi upinde ulivyo kwa mshale wake shujaa wa vita. Njia ya kurusha na mwelekeo ambao upinde wake unarusha mishale yake, hutengemea uwezo wa kutupa na mwelekeo ambao mshale utokapo katika upinde.

Watoto wetu ni mishale nao wazazi ndio upinde ambao watoto hao hurushwa nje katika ulimwengu. Tunapotambua changa moto inayotukambili kama wazazi, ni lazima turudi katika mistari hii miwili ya kwanza inayofungua na tukumbushwe kwa msemo kwamba hatuwezi kuijenga nyumba isipokuwa Bwana awe mjenzi.

Fumbo lingine lenye kuvutia linadhihirisha kweli hii kwamba hatuwezi, ila Mungu anaweza kuijenga ndoa na jamii. Yeye huwapa wapenzi wake usingizi, kulingana na Sulemani. Wakati wote tungali macho na kujaribu kumsaidia Mungu kutupatia nguvu katika miili yetu, Mungu hawezi kutuhuisha katika utu wa kimwili. Lakini, wakati tunapojiachilia na kwenda katika usingizi, Mungu anafanyika mtendaji na kuihuisha miili yetu iliyochoka nafsi, hisia pamoja na roho zetu.

Ndoa Yenye Thamani

Jinsi mchoro wetu wa pembe tatu unavyodhihirisha, wazazi wenye thamani ni matokeo ya watu wamchao Mungu ambao wamo katika ushirika uliochaguliwa Naye. Ili ndoa iendelee kuwa thabiti, na ili kwamba wazazi wawe na uwezo katika kuwalea watoto wao, - ni lazima Mungu awe kina cha uhusiano wa ndoa yao. Sisi hatuwezi kutenda wajibu wetu wa ndoa na uzazi, Mungu asipotusaidia.

Haya yote yanapatikana katika **Mathayo 19**, ambapo Yesu alikuwa akiulizwa kuhusu ndoa na talaka. Yeye anatambua kwamba Musa aliwakubalisha talaka, lakini hii ilikuwa kwa ulinzi wa wanawake ambao waume zao walikuwa wakiwatenga nje ya nyumbani. Katika siku zile, wanawake hawakuwa na haki zo zote. Hawakuwa na fidia ya talaka. Na kwa sababu ya huruma yake kwa wanawake, Musa aliwapa Waisraeli ruhusa ya talaka, lakini haikuwa kusudi la Mungu, kulingana na Yesu Kristo. Kusudi lake Mungu hapo mwanzo lilikuwa kwamba kusiwepo na talaka.

Kisha mmoja wa mitume - yamkini alikuwa ni Petro - alisema, '*mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo, haifai kuoa'* **19:10).** Yesu akajibu, '*Si wote wawezao kulipokea neno hili, ila wale waliojaliwa'* **(11)** - kumaanisha, ni wale tu ambao Roho Mtakatifu atawaangazia na kuwasaidia kuelewa na kuyatenda mafundisho hayo. Bila usaidizi wa Mungu, Yesu alikuwa akisema, haiwezekani kufanyika mshiriki mtimilifu katika ndoa.

Sulemani na Yesu wanatuambia, kuwa bila Mungu, haiwezekani kujenga nyumba zetu. Sisi hutenda kazi bure bila Yeye. Hatuwezi kuwa wazazi wakamilifu bila nguvu zake Mungu, na hatuwezi kuwa washirika wakamilifu bila usaidizi wa Mungu. Mafundisho yote ya Maandiko ni kwamba hatuwezi kuwa wakamilifu bila usaidizi wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili, kulingana na Yesu. **(Yohana 3:6).** Mwili ni asili ya mtu bila usaidizi wake Mungu. Yesu alituambia kwamba bila Yeye, hatuwezi kutenda lo lote. **(Yohana 15:5).**

Ikiwa ungelipenda kuwa na ndoa mbele yake Mungu, ndoa iliyoletwa pamoja na kutayarishwa na Mungu, ndoa ambayo itatimiza makusudio yake Mungu, basi yafanye maombi haya:

'Ee Baba wa mbinguni mpendwa, Yabariki makao haya.
Ibariki nyumba yetu na mwangaza wa uwepo wako.
Tuwezeshe na upendo wa Roho wako
Uhusiano ambao huijenga nyumba hii kuwa ni jamii.

Tuponye kama watu binafsi, ili kwamba tuwe na ushirika mkamilifu.
Na tuwe wazazi wenye hekima na upendo
Tufunze jinsi ya kuisongelea neema Yako siku nzima, na kila siku.

Twaomba kila kitu tufanyacho katika nyumba hii
Kifanyike katika Kristo, na Kristo, na kwa Kristo.

Mwanga wako, na uzima wako, na upendo wake Kristo aliyefufuka anayeishi
Utuwezeshe na kutuongoza
Ili tuwe waakilishi wake Kristo
Tunapoingia ndani, tunapo toka nje, na
Hasa tunapoishi pamoja ndani ya kuta hizi.

Ifanye nyumba hii kuwa ishara ya tumaini
Ambayo itamwelekea Yeye
Ambaye aliiweka nyumba hii pamoja katika Neno Lake
Aliyeileta pamoja kwa Roho Wake,
Na ambaye huiweka pamoja kwa neema Yake.

Katika jina la Yesu, Baba, ibariki nyumba yetu. Amina.

Sura ya 2

Ndoa Machoni Pa Mungu

Kuna kifungu katika vitabu vya Injili ambapo tunapata mafundisho dhahiri kutoka kwa Yesu kuhusu ndoa na talaka. Tayari tumegusia kifungu hiki lakini ni lazima tukirudia hivi sasa kwa kuwa kinamwonyesha Yesu akimnukuu Musa na kutoa jibu kwa Agano la Kale na Jipya kwa swali, 'ndoa ni nini machoni pa Mungu?'

'Baadhi ya mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu, wakimwambia, je! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu? Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.'

'Wakamwambia, Jinsi gani, basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha? Akawaambia, Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi. Nami nawaambia ninyi, kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya usherati, akaoa mwingine, azini'

'Wanafunzi wake wakamwambia, Mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo, haifai kuoa. Lakini Yeye akawaambia, Si wote wawezao kulipokea neno hili, ila wale waliojaliwa' **(Mathayo 19:3-11).**

Ndoa Ni Ushirika Wa Maongozi Ya Mungu

Moja ya hatua saba za uhusiano huu, kama nilivyowaeleza katika sura ya 1, ni kwamba kuna hatua ya maongozi ya Mungu katika ushirika wake mume na mke. Katika sura ya uumbaji kwenye Biblia, tunaona Muumbaji akiwaleta mwanamume na mwanamke katika 'Umoja.' Yesu alifafanua ndoa mbele za macho ya Mungu wakati aliposema, 'Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.' Ndoa ni ndoa mbele ya macho yake Mungu wakati tuwezapo kusema kwamba Bwana amewaunganisha mwanamume na mwanamke pamoja. Uongozi wake Mungu unapaswa kuwa msingi wa uamuzi wetu katika kuoa.

Basi ushirika ni maongozi ya Mungu kwa sababu Aliuweka ushirika huo pamoja wakati alipotupatia nakala yake katika Neno lake. Mungu aliwaleta hawa watu wawili pamoja wakati alipowafanya kuwa mwili mmoja, naye Yesu anatuambia kwamba ni Mungu peke yake awezaye kuwaweka pamoja.

Kwa sababu kila mshiriki huleta shida zake katika uhusiano wa ndoa, changa moto iliopo ni sisi tujione wenyewe katika ndoa- jukumu, wajibu na nyadhifa zetu ambazo tunahitajika kuchukua. Tunahitajika kuona mchango ambao tunapaswa kufanya katika ndoa na kuhusika ikiwa tunafanya au hatufanyi mchango wo wote. Na kwa upande mwingine, tunahitajika kuwajibika kwa sababu ya shida zile tunachangia katika ndoa.

Ndoa Ni Shirika La Kudumu

Kutokana na mafundisho ya Yesu katika Injili ya **Mathayo 19**, tunaona kuwa ndoa ni sharti la uhusiano wa kudumu maisha. Basi kwa nini ndoa iwe uhusiano wa kudumu maisha? Jibu linaweza kujumlishwa katika maneno haya: Haki za Watoto.

Kumbuka mfano wa maelezo kuhusu ndoa ambayo Sulemani alitupatia katika **Zaburi 127?** Wazazi ni kwa watoto, jinsi ilivyo upinde ni kwa mishale. Kipimo cha uwezo wa mvuto na upande ambao watoto huelekea katika maisha unatengemea upinde ambao walivumwa kutoka kwake. Kama ungelikuwa Ibilisi na unataka kuvunja jamii, je, ungefanya nini? Ungekata kamba ya upinde huo? Ungevunja ule upinde? Hivi ndivyo hakika Ibilisi anavyofanya. Yeye amejitosa kwa bidii huku akijaribu kuziangamiza jamii, kwa kukata kamba kwenye upinde.

Sheria ya maisha ambayo Mungu aliunda kwa ajili ya ndoa na jamii ni mojawapo ya amri za kale katika Biblia kwa sababu huijenga nyumba ambayo bila shaka huwapa watoto miaka kama ishirini ya malezi kabla yao kujiunga na ulimwengu na kukumbana na maisha. Wao wahitaji malezi na usalama. Unapoikata kamba katika ule upinde, wakati ndoa inapovunjika, basi unawanyang'anya watoto wako usalama na malezi, pamoja na mwelekeo ambao Mungu alikusudia wakati alipoandika sheria ya ndoa na jamii katika sura mbili za kwanza za Biblia. Hii ni moja wapo ya shida kuu ambazo watoto wakakumbana nazo siku hizi. Mshauri mmoja mkongwe mwenye umri wa miaka sabini na minane ambaye amewashauri vijana maishani mwake aliyanena haya, 'Kwa mara ya kwanza katika ujuzi wangu wa ushauri, vijana wadogo waniuliza swali hili, 'je, nawezaje kuwaweka watu wangu pamoja?'

Hii ndio sababu Yesu alisema, kuwa ndoa ni sharti iwe uhusiano wa kudumu milele. Watoto wako wana usalama tu kulingana na ndoa yenu ilivyo, na wanafahamu hivyo hata bila kuelezwa. Ikiwa unataka kuona hofu nyusoni mwa watoto wako, watazame wakati unapogombana na mwenzio. Wanapowaona baba na mama mzazi wakigombana, wao hujihisi bila usalama kamili. Kwa upande mwingine, ikiwa ungependa kuona furaha kwenye nyuso zao, basi mwonyeshe mwenzio upendo; hata mbusu mbele ya watoto wako. Wao watakufanyia mzaha unapofanya hivyo, lakini usikubali kupumbazwa na jambo hilo. Kwa hakika, wao hupenda jambo hilo! Wanapokuona ukiudhihirisha upendo na wema, yaonekana kwao kwamba ndoa yenu inanawiri, na jambo hili huwapa usalama.

Wakati mwingi watu huwa katika ndoa ya pili au ya tatu wanapokuja kwa imani ndani ya Kristo. Wakati wanapoingia katika imani, wao huwa katika ndoa nyingine na wanao watoto kutoka ndoa zilizotangulia. Je! Mafundisho yake Yesu kuhusu ndoa na talaka yanawahusu na kuwagusa kwa njia gani watu kama hawa?

Kila mara Yesu alipitisha sheria yake Mungu katika kiio cha upendo kabla ya kuijumuisha hiyo katika maisha ya watu. Tofauti yake na wale wakuu wa dini wa siku zake ni kwamba, yeye hakupoteza kweli kwamba sheria yake Mungu ilitoka katika moyo Wake kwa upendo wa mwanadamu. Kusudi la sheria yake Mungu katika Maandiko kwa mwanadamu ilikuwa kueleza upendo Wake kwa mwanadamu. Mungu hututakia mema. Hii ndio sababu alitupatia Neno Lake Takatifu. Yeye hakuwa akijaribu kuangalia jinsi angetufanya kuadhirika kwa kutupatia sheria. Yeye anatutakia kuwa na furaha. Kuna kusudi kwa kila sheria ya Mungu katika Maandiko, na humjia vema mwanadamu kwa kuwa Mungu ampenda.

Mafarisayo, viongozi wa dini, walipoteza mtazamo wa sheria. Wao walifurahia kuwashika watu walioteleza na kuvunja sehemu ya sheria. Lakini Yesu hakupoteza mtazamo wa kusudi lake Mungu wakati alipotoa sheria kupitia Musa. Wakati wote Yesu alitilia mkazo jambo hili, 'Kwa nini Mungu alileta sheria? Na ni kwa namna gani sheria hii inatueleza upendo wake Mungu kwa mwanadamu na kwa ajili ya wema wake mwanadamu?'

Kusudi la sheria ya ndoa na jamii, kwa mfano, ni kwamba tuweze kuwa na jamii yenye furaha yenye kumtumainia Yesu. Tunasoma katika maelezo ya uumbaji kwamba sio vema kwake

mtu kuwa peke yake na jambo hili lilimpa Mungu motisha kuwaweka wenye upweke katika jamii **(Zaburi 68:6).** Yeye hataki sisi kuwa peke yetu. (Kwa maelezo zaidi tazama sura ya 6 ya kitabu hiki).

Ndoa Ni Uhusiano Wa Kipekee

Bali na ndoa kuwa maongozi ya Mungu na uhusiano wa kudumu, kulingana na Yesu na Musa, ni lazima iwe uhusiano wa kipee. Umoja kati ya mume na mke ni wa hisia mbili za kipekee. Musa aliandika: 'Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye,. . .' Yesu akubaliana na Musa alipotoa maelezo haya sahihi kuhusu ndoa na jamii **(Mathayo 19:5**). Ndoa haiwahusishi wazazi wa hao waliooana. Hii haimaanishi, kwamba hauwezi kuwa na uhusiano mwema na wazazi wako unapoifunga ndoa. Lakini inamaanisha kwamba hautaishi katika nyumba yao tena. Ikiwa wewe ni mwanamke, baba mzazi wako atakuwa siye mkuu wako wa kiroho tena; bali ni mumeo.

Ndoa pia ni ya kipekee kwa njia nyingine nyeti. Yesu alifunza kuwa ndoa ni kama mkataba au maagano kati ya mwanamume na mwanamke. Sharti la maagano ye yote ni hali ya kipee au kutohusisha. Hali hii inapovunjwa, mkataba wa ndoa unaweza kutambulika kama batili na uliotanguka. Sio lazima jambo hili litokee, lakini inawezekana. Mungu hakufanya ndoa hivi kwamba ye yote anaweza kuishi na mwenzi ambaye hawezi kuishi katika uhusiano ule bila kuwahusisha wengine au pekee. Mungu hataki wewe utende hivyo. Ikiwa mwenzio hawezi kuishi na wewe bila kuwahusisha wengine katika uhusiano huo, basi unaweza kutangaza huo mkataba kuwa batili na uliotanguka, kwa sababu kulingana na Yesu, ndoa ni uhusiano usiohusisha wengine au wa kipekee.

Wakati mmoja mtu aliyekuwa akifanya kazi katika hoteli karibu na bahari, alimtembelea mchungaji ambaye alikuwa kiishi karibu na hoteli hiyo. Yeye alikuwa amekutana na msichana mmoja katika msimu wa hari au wa jua kali na akampenda sana. Yule mtu alikuwa na uhusiano wa kimapenzi kipindi chote cha hari pamoja na yule msichana. Wakati majira ya hari yalipofikia mwisho, yule msichana alirudi kwenye chuo kikuu, lakini angemtembelea mwishoni mwa juma kila mara akipata fursa. Ikawa siku moja mwisho wa juma hakuja kumtembelea. Msichana yule alimpigia simu na kumwambia kwamba hatamtembelea tena.

Yule mtu aliketi afisini mwa mchungaji huyo akiwa mwenye machozi huku moyo wake ukiwa umevunjika. Mwishowe, alisema hivi, *'unajua, uhusiano kama huu, ambao hisia zake ni nyingi na kuu, unahitajika kuwa na ulinzi fulani.'* Alizidi kulia huku akisema kwamba hataki kuweka hisia zake zote katika kitu ambacho hakina usalama wa aina ye yote ile, jambo ambalo lingekwisha kwa kijikaratasi kidogo cha ujumbe kilichotupwa chini ya mlango au kupigiwa simu - au hata kukosekana kwa kijikaratasi au kutopigwa kwa simu ili kupashwa habari. Yeye alikuwa tayari kusikiliza uhusiano wa ndoa ambao nakala yake ilitayarishwa na Musa na idhinisho ambalo Yesu alihakikishia kwa ufasaha.

Mungu hataki wewe huwe bila usalama katika uhusiano wako wa ndoa. Hii ndiyo sababu Yesu na Musa walifanya sharti ‘la kipekee au lisilohusishwa’ la agano la ndoa.

Sura ya 3

Pete Au Viunganishi Saba Vya Umoja

Mcha Mungu mmoja wa asili ya Kiafrika alichonga sanamu moja ya kuvutia inayoonyesha uhusiano ambao Mungu alikusudia wakati alipowaumba wenzi wa kwanza na kuwatangaza kuwa ni ‘Mwili mmoja.’ Wakati mwaminifu huyu mwenye kipawa alipochonga mfano huu, alikuwa akionyesha njia au hatua saba ambazo mume na mke wanahitajika kuwa mwili mmoja.

Nakshi au sanamu hiyo yake ya kuvutia ni mwanamke na mwanamume waliochongwa kutoka kwa kipande kimoja cha mti. Wameunganishwa kwa mnyororo wa pete wenye viunganisho vitano viwili viwili. Mnyororo huu wenye kuwaunganisha pamoja pia umeunganishwa na kiunganishi ambacho kiko kwenye vichwa vya kila mmoja. Kila moja ya viunganisho hivi ni ishara ya sehemu ya umoja wao ambao Mungu alikusudia kwa mume na mke. Kiunganisho kilicho juu ya vichwa vyao kinawakilisha uhusiano wa kiroho walio nao kila mmoja kwake Mungu. Hali kwamba pete nyingine zote zimeunganishwa kwa viunganisho hivi viwili inawakilisha uthibitisho kwamba uhusiano wa kiroho ndio msingi wa umoja wao.

Pete mbili za kwanza zinawakilisha mawasiliano, ambayo ndiyo chombo kinachowawezesha kuazisha na kudumisha umoja wao. Pete ya pili ni usawa, ambao ni ushahidi wa umoja wao. Pete za katikati ya hizi tano zinawakilisha upendo, ambao ndiyo nguvu na kasi ya umoja wao. Pete ya upendo inafuatiwa na ile ya ufahamiano au uelewano, ambayo inawakilisha kukua kwa umoja wao. Pete za mwisho katika viunganisho hivi ambavyo huwafanya kuwa mwili mmoja ni ngono au kujamiiana, ambayo ni kielelezo cha furaha kinachodhihirisha umoja wao. Hali kwamba viunganisho hivi ni vyenye pete mbili mbili inawakilisha uhakika kwamba sehemu hizi zote za umoja vyabadilishana, au vinahusu kutoa na kupokea kati yao. Unapojumuhisha pete hizi kwa viunganisho vilivyomo kwenye vichwa vyao, basi una viunganisho au pete saba za umoja.

Pete Au Kiunganishi Cha Kiroho

Wasomi wa Biblia wanaamini kwamba mfalme Sulemani alikuwa akitupa mtazamo kuhusu ndoa wakati alipohubiri kwamba kamba yenye nyuzi tatu haikatiki kwa haraka **(Mhubiri 4:12).** Kamba au amari yenye nyuzi tatu ni ngumu sana kukatika kwa sababu nyuzi zile zimeshikamana na zinaongeza nguvu nyingi.

Wakati Mungu alipounda umoja kati ya mume na amke ambao ni maongozi yake ya, kudumu na ya kipekee yanaohusisha wengine, alimaanisha kwamba wao wanapaswa kuwa mmoja kwa yule mwingine na kwa muumba wao. Hivi ndivyo Mungu alivyokusudia ndoa kuwa. Kuna mifano ya kuvutia sana ambayo unaweza kupata katika jiwe la makaburi la watoto wa Israeli hata siku ya leo: ‘.....*itafungwa katika furushi ya uhai pamoja na Bwana Mungu wako*.....’

(1 Samuel 25:29). Hii inafanya kibandiko kinachofaa sana kuandikwa kote katika kila ndoa mbele yake Mungu leo. Nyuzi zile tatu katika mifano yake Sulemani zinaweza kuwakilisha ndoa ya waaminifu wawili kwa njia hii: Mume, Mke na Kristo.

Katika sura kuu ya ndoa, mtume Paulo, anawashauri wenzi wamchao Mungu kujitenga kwa muda mfupi ili wajitolee kwa maombi na kufunga. Kwa hakika yeye anazungumzia kuhusu uhusiano wa ngono kati ya hawa wenzi wawili. Wazo lake ni dhahiri kabisa kwamba uhusiano wao wa ngono pamoja na umoja wao unatiwa nguvu na umoja wa kiroho na Muumba wao **(1 Wakorintho 7:3-5).**

Tutauzungumzia umoja wa kimwili baadaye, lakini kwa sasa, ningependa kutoa maoni kuhusu yale Paulo anayodhamiria katika kifungu hiki kuhusu mambo yaliyo nyeti katika uhusiano ya maisha yako. Mambo ya karibu sana na nyeti katika maisha yako sio kati yako na mke au mume mwenzio, ila ni uhusiano kati yako na Mungu. Paulo anafundisha kwamba uhusiano wetu na Mungu ni wa karibu sana, wa kibinafsi na ulio muhimu sana.

Ikiwa ndoa itatiwa uthabiti kwa kujitenga kwetu na kwa ubinafsi kumkaribia Mungu, hii inamaanisha kwamba tungali tukishirikiana na Mungu kibinafsi hata kama tungali kwenye hali ya ndoa na wenzi wetu. Ikiwa utalifikiria jambo hili, tutakapo simama mbele yake Mungu katika hukumu, itatubidi sote kujitetea kibinafsi Kwake, sio kwa niaba ya wenzi wetu. Tutasimama mbele ya Kiti cha Hukumu binafsi, wala sio kwa pamoja kama mtu na mkewe. Ndoa ya watu waaminifu wawili ni thabiti au dhaifu kulingana na umoja wa ubinafsi uliopo kati yao na Mungu. Ikiwa mume ana imani thabiti na uhusiano pamoja na Kristo, sawa na mke, wanapokuja pamoja, wao huwa kitu sawa - wana sehemu ya kiroho katika ndoa yao ambayo itawapa nguvu zaidi katika uhusiano kwa mwingine.

Wakati mume na mke wanapokuwa na wakati wa kimya mbele za Mungu kwa maombi, kusoma Biblia na kuabudu, hii itawasaidia kupitia nyakati ngumu. Mara kwa mara wanaweza kukosana kwa labda yale mmoja wao aliyanena au kutenda, lakini wanaporejea kutoka muda wa kimya mbele za Mungu, watakuwa katika imani na Bwana - na kati yao wenyewe. Wote wanapozidi kusongea karibu na Bwana kila siku, watashuhudia ukuaji wa karibu na Mungu na hata kati yao.

Ikiwa hauko karibu na mwenziwe jinsi ungetaka, basi binafsi, mkaribie Mungu. Hivi ndivyo kiunganishi cha kiroho cha umoja kilivyofanywa kuipa ndoa nguvu ua uthabiti. Kwa sababu mume na mke wana kiunganishi hiki pamoja na Mungu, naweza kusema kwamba viunganishi hivi ni msingi wa ndoa ambayo Mungu ametoa nakala yake katika Biblia.

Sura ya 4

Kiunganisho cha Mawasiliano

Wakati wenzi wanapokutana na mchungaji au mshauri wa ndoa, shida ya kwanza wanayoitilia mkazo ni mawasiliano. Wakati mwingi wao huanza kikao chao kwa kusema, *'Sisi hatuna mawasiliano. Sisi hatuwasiliani.'*

Mawasiliano ni hatua ya ndoa ambayo linaweza kuwasaidia hao wawili kufanyika mwili mmoja kwa sababu ni chombo ambacho huwezesha kuendeleza umoja. Kama waaminifu waliozaliwa mara ya pili, tuna umoja na Kristo. Umoja pamoja na mwokozi haujitoshelezi tu wenyewe. Ni lazima udumishwe. Ni lazima upaliliwe. Hii ndiyo sababu lazima utumie wakati wako kila siku pamoja na Bwana katika maombi na kusoma Neno lake Mungu. Kwa maelezo mengine, sisi hudumisha na kupalilia uhusiano wetu na Kristo kwa kuwasiliana naye katika maombi na kuisikiliza sauti Yake wakati tunapoifungua Biblia yetu.

Jambo hili pia ni la kweli katika ndoa. Ni lazima tudumishe na kupalilia uhusiano wetu. Mawasiliano ni chombo ambacho wenzi wanaweza kutumia katika kupalilia na kudumisha umoja wao. Viini vya bakteria huzaana na kuongezeka kwenye giza, lakini haviwezi kuishi katika nuru. Ikiwa watu wawili hawawasiliani, 'viini vingi vya bakteria' vitazaana kati yao. Hii ndiyo sababu Paulo anatuhimiza *'kuyakataa mambo ya aibu yaliyositirika wala tusienede kwa hila.'* Tunapokuwa wenye hila na kuyaficha mambo kutoka kwa wenzi wetu, huwa tunaweka 'viini vya bakteria' kwenye giza. Mawasiliano ni sawa na kuangaza nuru katika uhusiano wetu. Tunapofanya hivyo 'viini vingi vya bakteria' hufariki. Kupitia mawasiliano mema, tunaweza kuyazungumzia yale yasio kufa vile 'nuru' wa mawasiliano inapokuwa chombo cha kupalilia na kudumisha umoja wetu.

Kamusi hufafanua mawasiliano kama 'kupeana na kupokea habari, ujumbe na mawazo kwa kuzungumza, kwa ishara ya mikono au kwa njia zingine.' Ufafanuzi huu unatueleza mambo kadhaa kuhusu mawasiliano. Kwanza, hakuna kitu kama 'hakuna kuwasiliana.' Wakati watu wanaposema kwamba, 'Sisi hatuna mawasiliano,' huo sio ukweli. Tunawasiliana wakati wote; tofauti ni jinsi gani tunavyowasiliana na kile tunachowasiliana? Kuzungumza? Kutumia ishara ya kupungiana mkono? Au kwa njia zingine zile?

Ufafanusi huu wa mawasiliano pia unaeleza kwamba kuna hatua mbili katika mawasiliano; kupeana na kupokea. Mwanamke mmoja aliwahi kusema haya, 'Ni kana kwamba mume wangu anaishi katika kisiwa cha ajabu kisichojulikana nami nimekuwa nikizunguka kisiwa hicho kwa miaka ishirini na siwezi kupapata mahali pa kuengeshea jahazi langu kwenye kilindi.'

Hebu fikiria kwamba wewe na mwenzio mko kwenye visiwa tofauti na mnawasiliana kwa njia ya redio. Ili kuwasiliana kwa redio, ni lazima mmoja awashe redio yake ndipo aweze kutuma ujumbe, naye mwenzake anahitajika pia aiwashe redio yake ili kupokea ujumbe huo. Wakati mwingine, matatizo ya mawasiliano yanaweza kupatikana kwa kweli kwamba mmoja wa wenzi hao hawezi kuwasha redio yake na kuwasiliano na mwenzake. Na wakati mwingine, wanapotuma mawasiliano yao, ujumbe wao huwa haufahamiki kwa kuwa unachanyikana. Pia kuna wakati ambapo shida za mawasilano zinaweza kupatikana katika hali ambapo mmoja au wote katika uhusiano huu hawakuwasha kifaa cha kupokea mawasiliano, au wakati wanapofanya hivyo, vifaa hivyo vimewekwa katika masafa tofauti.

Jinsi ujumbe unavyopokelewa ni muhimu kama ilivyo mawasiliano yanavyotumwa. Wakati kobe anapotoka kwenye kono lake, ikiwa utamkanyaga, basi atarudi ndani na kujificha hapo kwa muda mrefu. Hebu fikiria kwamba kuna jambo ambalo unalishiriki kwa siri pamoja na mwenzio. Ikiwa ujumbe ule haukupokewa vyema, basi wewe utajitumbukiza ndani ya kono lako na utakaa vivyo hivyo kwa muda mrefu.

Ikiwa huwezi kuwasiliana vyema, basi hauna chombo cha kupalilia na kudumisha umoja wenu. Hauwezi kutenda lo lote katika uhusiano wenu. Inawezekana kuendeleza mawasilano yako vyema na kuwa na chombo hiki ambacho hukuwezesha kutenda kazi katika ndoa yako.

Tofauti na uhusiano wa mzazi na mtoto, ambao mara nyingi huanza wakati wa kuzaliwa na huwa na wakati wa kutengana, uhusiano wa ndoa huwavuta watu wawili pamoja. Ndoa imefanywa kuwa kama lile jengo la pembe tatu zinazoungana na kufanyika moja. Mawasiliano hutupatia chombo ambacho hutuwezesha kufanya hivyo. Ikiwa wenzi wawili hawana mawasiliano mema, basi wao hawana chombo ambacho Mungu amekiunda ili kuwawezesha kuendeleza uhusiano wao.

Shida za mawasiliano huja kwa namna mbili. Namna moja ni katika ugomvi. Baadhi ya wenzi hawawezi kuwasiliana kwa dakika tano bila ugomvi juu ya jambo fulani. Namna nyingine ni kinyume na iliyotangulia - Kimya. Watu huwa tofauti, watu wengi huwa hawana faraja kwa kimya. Kwao kimya ni kibaya. Wengine ni wale ambao 'ni wa kimya' na hawahitaji kuzungumza.

Kuna mtu mmoja ambaye hupenda sana kukaa kimya. Basi siku moja mke alimwendea na kumwambia, *'Wewe hauna mengi ya kusema, sivyo?'* Naye akajibu, *'Wakati maji ni mengi, huwa tulivu na kimya. Lakini yakiwa haba, hutoa povu.'* Huyu mtu hakuwa akimdharau huyu mama ila tu alikuwa akimpasha ujumbe.

Hivyo basi, ikiwa wewe ni mmoja wa wale wenye kimya kikuu, hiyo haimaanishi kwamba una shida ya mawasiliano. Njia moja ya kuvutia ni kuwa na ushirika ambao ndio shina la neno mawasiliano. Inawezekana kufarijika pamoja hivi kwamba sio lazima kuwasiliana ili kuwa pamoja. Kimya hakimaanishi wakati wote kwamba kuna shida ya mawasiliano.

Hata hivyo, 'udhilifu wa kimya' ni aina ya mawasiliano, na inaweza kumaanisha kwamba una shida ya mawasiliano. Ikiwa mwenzio anakuonyesha udhilifu wa kimya, hiyo inamaanisha kwamba umemkasirisha na anatumia kimya ili kuwasiliana nawe. Mwanamke mmoja ambaye mumewe alikuwa akitenda hivyo alisema hivi, *'Ni lazima umkaribie karibu sana ili kukisikia kile ambacho anakisema wakati anapozungumza.'*

Sisi huwasiliana kwa njia ya kuzungumza, kwa ishara kama kupunga mikono au kwa njia nyingine. Njia zingine zinaweza kuwa ni kimya, kutupiana sinia, kugonganisha mlango, au kupiga ukuta ngumi. Na kwa upande mwingine wakuvutia, tabasamu, kuwekelea mkono juu ya bega, kukumbatia au machozi. Hivyo basi, unaweza kuona kwamba hakuna jambo kama

kutowasiliana. Wakati mwingi sisi huwasiliana kupitia ishara au kupunga mikono ilhali wakati mwingine bila maneno, lakini njia hizo zingine ni mawasiliano yenye ufasaha sana. *Francis Assisi* alisema wakati mmoja kuwa, *'katika mambo yote, hubiri Kristo. Na ikiwa ni lazima, tumia maneno.'* Mawasiliano sahihi, yakiwa mema au mabaya, hayahitaji maneno wakati wote.

Yupo mwalimu mmoja wa mawasiliano aliyeingia kwenye darasa lililokuwa na kelele mingi sana. Alikwenda moja kwa moja hadi mezani mbele ya darasa na kuligonga kwa ukofi juu. Kishido chake kilikuwa kama mlio wa bunduki, na alipokuwa akigonga kwa ukofi huo, alipaza sauti ya juu hivi, 'Nataka ghasia kamili!' Wanafunzi walikimya kabisa. Kisha aliwaeleza kwa nini alifanya hivyo. Asilimia saba ndio maneno. Asilimia hamsini na tano ya mawasiliano ni namna ya sauti ambayo tunaitumia tunaposema maneno hayo, na asilimia thelathini na nane ni jinsi ishara ya miili yetu inavyofuatana na maneno tunayonena. Yeye alikuwa amesema, 'nataka ghasia kamili!' Lakini hilo halikunyamazisha wanafunzi wa darasa hilo. Ikiwa wanafunzi wangeelewa kile alichosema, hiyo ingekuwa matokeo tofauti. Badala yake, kile kilichonyamazisha darasa ni namna au njia ile ambayo aliyanena maneno hayo. Na kwa sauti yake, wanafunzi walifahamu kwamba alikuwa akisema, *'Nataka kuwe na utaratibu katika darasa hili!'* na hilo lilitiliwa mkazo wakati alipogomga meza kwa nguvu.

Kwa Muhtasari

Mawasiliano sio tu yale tunayoyanena; bali ni yale tunayosikia. Mawasiliano sio yale yanayonenwa tu; bali pia ni yale tunayoyapokea. Mawasiliano sio yale yanayosemwa, bali pia ni yale tunayohisi kulingana na ishara na njia zingine zile. Mawasiliano sio yale yananenwa tu; bali pia yale watu wataka kusikia. Mambo haya yote humwacha mpokeaji na 'ufahamu wote' wa kile kilichowasilishwa kwa kunena, kwa ishara, na kwa njia nyingine.

Shida Za Mawasiliano

Kama mchungaji kwa siku nyingi, nimekuwa nikiwauliza wenzi, 'Je! Mna mawasiliano bora?' Wakati mwingi bila kusita jibu limekuwa 'Ndio.' Nimewapa kazi ya kufanya. Ikiwa shida yao ilikuwa kwamba wao hawazungumzi tena, ningewauliza kunakili orodha ya sababu ile iliyowafanya kuacha kuzungumza na wenzi wao. Ikiwa shida ilikuwa kwamba hawangeweza kuwasiliana bila kukasirikiana, ningewauliza kunakili orodha ya sababu iliyowafanya kukasirika wakati wanapokuwa wakizungumza na wenzi wao. Nilizitaja shida hizi kama 'pingamizi za mawasiliano.'

Kwa miaka mingi nimekusanya orodha hizo na kuzisoma. Katika nakala za orodha hizo, nimegundua na kutambua zaidi ya shida ishirini za mawasiliano zilizoibuka katika nakala hizo. Hapa kuna baadhi ya dondoo za shida hizo; hebu tazama ikiwa unaweza kutambua baadhi yake:

1. **Kutopendezwa.** Mke mmoja alinakili kwamba alimwambia mumewe jioni moja kuwa, 'Mtoto alikipata kidole chake cha gumba leo.' Yeye alikuwa na msisimko mwingi sana kwa maendeleo ya yule mtoto, lakini mumewe hakuwa akimsikiliza. Yeye alikuwa angali kazini kwenye mawazo yake au alikuwa akisoma gazeti. Hakuna mtu anayetaka kuwasiliana wakati anapotambua kwamba anajizungumzia mwenyewe. Na lililo mbaya kuliko

kutosikiliza linamaanisha jambo lingine lenye uzito mkuu - kutopendezwa. Hii inasema kwa yule mke kuwa, ‘Mimi sipendezwi nawe wala yule mtoto.’ Kulingana na yule mwanamke, kutopendezwa kwake kunamaanisha kwamba hampendi wala yule mtoto.

2. **Hakuna Mwingizo.** Kumbuka mawasiliano ni kupeana na kupokea. Siku moja mmoja wao anatambua kwamba, ‘Mimi ndiye mwenye kupeana tu. Yeye hachangii cho chote katika mawasiliano yetu. Yale atendayo ni kupokea tu.’ Ikiwa mawasiliano ni daraja, mume na mke wahitajika kukutana katikati. Ikiwa mmoja wao ni lazima aendelee kulijenga daraja lote, basi yeye huvunjika moyo na kuacha kujaribu.

3. **Mwenzio Mwenye Ugomvi Na Ubishi.** Sulemani alisema kwamba mwanamke mgomvi ni sawa na kutona-tona daima siku ya mvua nyingi **(Mithali 27:15).** Hakika, wanaume na wanawake watoshana kuwa wabishi na wagomvi. Mtu mgomvi au mwenye ubishi hushindana na kila kitu ambacho mwenzi wake anasema. Ukiibuka na wazo jipya, mtu mwenye ubishi wakati wote atalipinga. Ni vigumu sana, na wakati mwingi inaonekana kana kwamba haiwezekani kuwasiliana na watu wenye ubishi.

4. **Kushindwa Kutambua Haja La Mwenzio La Faragha.** Haidhihirishi ubaya wo wote katika ukaribu wenu ikiwa mwenzio anataka nafasi ya faragha mwenyewe. Usitishwe na ukweli huo. Kumbuka, hata ikiwa ‘wawili watakuwa mmoja’ katika ndoa, kuna hali ya utendaji ambao sisi huwa wawili.

5. **Wakati Mwingine Shida Za Mawasiliano Zinasababishwa Na Mambo Ya Kimwili, Hisia, Na Kiroho Katika Mmoja Au Wote Wawili Katika Ndoa Ile.** Wakati hali inapokuwa hivyo, hakuna kiwango cha kusoma mawasiliano kinachoweza kusuluhisha shida hizo. Suluhisho kwa shida zile ni lazima zipatikane kwa njia ya kiroho, kimwili, na kihisia mara nyingi kutoka nje ya uhusiano.

6. **Shida Za Afya Huadhiri Mawasiliano Na Uhusiano Wa Watu Waliooana.** Wakati wote tilia maanani kwamba kuna uwekezekano kwamba shida ya kimwili ndiyo sababu ya ugumu wa mawasiliano. Hii ni kweli hasa wakati ambapo ni vigumu kwa watu kuwasiliana kinyume cha hapo awali. Shida za kihisia na kiakili pia zinaweza kuzalisha mabaya katika mawasiliano. Ikiwa mwenzio ana shida kuu ya kihisia au kiafya, ni lazima autafute usaidizi anaohitaji.

Suluhisho Kutoka Kwenye Maandiko

Wakati mwingine, shida kuu iliyopo ni uchoyo au kujifikiria tu. Mmoja wao au wote wawili hashughuliki na yule mwingine ila tu mambo yake mwenyewe. Hii ndiyo sababu yeye hahusiki wala hasikilizi. Wakati shida inapokuwa ya kujifikiria, suluhisho ni kutojifikiria. Kanuni kuu ndio suluhisho. Yesu alituamuru kutilia maanani yale tunayotarajia wengine kututendea kisha tuwatendee wao vivyo hivyo. **(Mathayo 7:12).** Fundisho hili kuu la Yesu linaweza kubadilisha

mawasiliano ya wenzi waliooana. Kila mmoja wao anahitajika kutojifikiria na badala yake kumfikiria mwenziwe na kushughulikia mambo ya mwenziwe pasipo na unafiki wo wote kwa mambo ambayo ni muhimu kwa mwenzio.

Matatizo mengi yaliyomo katika mawasiliano yanaweza kuepukika kwa kumwomba Mungu hekima. Mojawapo ya mstari ninaopenda sana ni **Yakobo 1:5,** ambao unasema hivi, *'Lakini mtu wa kwenu na akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu.'* Wakati wote tunahitajika kuwa tukimwomba Mungu hivi, *'mimi sifahamu ambalo nahitajika kulitenda. Ninahitaji hekima ambayo sina. Wewe umetuambia kutenda hivyo, nami nimetenda hivyo.'* Utashangazwa na jinsi Mungu anavyopendezwa na kuwapa watu wake hekima wanapomwomba hiyo hekima. Hivyo basi, wakati changa moto za mawasiliano zinapokuleta mahali ambapo haujui la kufanya, muombe Mungu hekima.

Jinsi Ya Kuwasiliana Na Mtu Mgumu

Kuna kifungu kingine ambacho kinatuonyesha jinsi ya kusuluhisha matatizo yaliyomo katika mawasiliano. Yasikilize mashauri haya ambayo Paulo alimpa Timotheo: *'Walakini uyakatae maswali ya upumbavu yasiyo na elimu, ukijua ya kuwa huzaa magomvi. Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu; akiwaonya kwa upole wao washidanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awape kutubu na kuijua kweli; wapate tena fahamu zao, na kutoka katika mtego wa Ibilisi, ambao hao wametengwa naye, hata kuyafanya mapenzi yake'* **(2 Timotheo 2:23-26).**

Ikiwa mwenzio ni 'mtu mgumu,' ni kana kwamba yeye amechukuliwa mateka na Ibilisi. Yuko katika kifungo cha Ibilisi na huwezi kumtoa katika kifungo kile. Ni Mungu peke yake awezaye kumweka huru.

Lakini hili ndilo uwezalo kulitenda ili kudumisha tunda la Roho. Tunda tatu za Roho zinatajwa katika kifungu hichi: Upole, uvumilivu, na saburi. Ukidumisha tunda la Roho Mtakatifu, hilo litaufanya mlango kuwa wazi kwake Mungu kutenda kazi kupitia wewe na kufunga mlango kwake Ibilisi. Hili litakupatia fursa ya kupokea usikivu na hatimaye kuweka mbele ya mwenzio kweli ambayo yaweza kumweka yeye au wewe huru. Paulo anamwonya mtumishi wake Bwana kwa dhati kwamba (wewe) inakubidi kutokuwa mgomvi au mwenye kushindana, kwa kuwa jambo hili huufunga mlango kwake Mungu na kuufungua kwake Ibilisi.

Huku katika hali ya maombi unapoyajumuisha mashauri yake Paulo kwa kuwasiliana na mtu mgumu, unahitajika wakati wote kutilia maanani kwamba inawezekana kuwa ndiye mwenzi mwenye ugumu. Yesu alisema haya katika **Mathayo 7:5,** *'mnafiki wewe itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako.'* Kuwepo kwa boriti au gogo katika jicho letu kunaweza kutufanya vipofu na kutukosesha kabisa kutambua kwamba sisi ndio tulio watu wagumu ambao Paulo anawaeleza katika kifungu kile.

Jawabu lingine la Kibiblia, hasa wakati mwenzio ana matatizo ya kihisia na akili au kimwili, ni kuomba maombi yale Yesu aliyoomba alipokuwa juu ya msalaba: *'Yesu akasema, Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo.'* Hebu fikiria: Katikati ya kifo chenye uchungu mwingi,

Yesu aliomba maombi ya aina hii kwa maadui zake. Ikiwa Yesu aliomba maombi ya aina hii kwa maadui zake, je! Si inawezekana kwako kumwombea hivyo mwenzi wako? Ikiwa wao hawaajibiki kwa yale wanayotenda kwa sababu ya matatizo ya kiakili, kihisia na kimwili kutokana na afya zao, miujiza ingetukia wewe kwa kuwafanyia maombi sawa na haya ya Yesu.

Mawasiliano Ya Kijamii

Ikiwa wewe na mwenzio mna watoto, eneo la mawasiliano ni kubwa kuliko wakati ninyi mkiwa wawili tu. Ni muhimu kutambua 'mchanganyiko mwingi wa mawasiliano' uliopo katika jamii na kuwa na wakati kwa ajili yake. Kwa mfano, mawasiliano yake mume na mke ndio muhimu sana katika jamii. Mengine ni kati ya baba na mama, ambayo ningependa kuwaeleza kama 'baraza la wakuu.' Usije ukayachanganya aina hizi za mawasiliano zilizo muhimu sana. Ufanye wakati wa mawasiliano kati ya mume na mke, na kufanya wakati mwingine kwa ajili ya mawasiliano kama wazazi.

La ziada, kuna mchanganyiko wa mawasiliano kati ya wazazi na watoto. Nyakati nyingi wanahitajika kupa umuhimu wa mbele au kipao mbele mawasiliano ya kibinafsi na kila mtoto, ilhali wakati mwingine kuwasiliana pamoja kama jamii nzima. Usisahau haja ya mawasiliano kati ya watoto pasipo na wazazi karibu nao. Labda umewahi kusikia ukiwa nyumbani pamoja na mke wako au mue wako watoto wenu wakiwasiliana mmoja kwa mwingine, na kuweza kuzitaja sauti zao kuwa 'Sauti za ndugu,' na hii inakuwa sauti ya wimbo katika masikio yenu.

Duara Ya Maisha

Hebu dhania juu ya mkate wa chapati uliogawanywa mara tatu. Acha kila kipande kiwakilishe theluthi moja ya maisha yako ya ndoa pamoja na watoto. Katika duara la kawaida la kimaisha, sisi hutumia takribani theluthi moja ya maisha yetu chini ya malezi ya wazazi wetu, theluthi nyingine tukiwapa malezi watoto wetu pamoja na wenzi wetu, na theluthi nyingine moja katika 'kiota kitupu,' wakati watoto wanapotoka nyumbani. Hii inamaanisha kwamba sisi hutumia theluthi mbili za maisha yetu pamoja na wenzi wetu. Uhusiano wa kimawasiliano katika maisha yetu ambao tunahitajika kuendeleza kwanza katika maisha ni kati yetu na wenzi wetu, kwa kuwa uhusiano huo utaendelea kwa muda mrefu zaidi baada ya watoto wetu kukua na kutuacha. Sababu nyingine ambayo mawasiliano haya yanahitajika kuwa jambo muhimu la kwanza katika maisha yetu ni kwamba uhusiano zingine zote hupata uharibifu ikiwa mawasiliano kati ya mume na mke yamevunjika.

Wazazi wengi hufanya kosa la kuwapa watoto nafasi ya kwanza. Ikiwa wao watapuuza uhusiano kati yao, wakati kiota chao kinapobaki wazi, wao wanaweza kutambua kwamba hawana uhusiano. Ni jambo la kuhuzunisha wakati ndoa zinapovunjika wakati huo kwa kuwa baba na akina mama walisahau kwamba wao walikuwa pia mke na mume. Mawasiliano yakupatia chombo ambacho kitaongeza nguvu katika uhusiano ulio muhimu sana nyumbani mwako

Sura ya 5

Kifungo Cha Utangamano

Utangamano ni ishara ya umoja ambayo Mungu aliunda kwake mume na mkewe. Dhana hii ya utangamano huwafanya watu wengi kufikiria usawa wa kimwili au kupumbaza. Utangamano wa kimwili ni wa muhimu sana, lakini utangamano haumaanishi tu kuhusu ashiki, bali unahusu mambo kama thamani zetu. Je! Thamani zenu zina utangamano? Hapa ndipo ndoa nyingi zinapokubana na utata. Wakati mwingi vijana wao huoana hata bila kuzungumzia kuhusu utangamano wao wa kiroho. Baada ya kuoana, mara nyingi wao hugundua kwamba hawana utangamano wo wote katika thamani zao za kiroho.

Kwa mfano, mke mchanga anapokuwa mja mzito na mumewe kumshauri kutoa mimba. Yule mke mchanga husema, *'Mimi sitalitenda jambo hilo. Hii ni kinyume na imani yangu.' Naye mume anasema, 'Imani yako inahusu vipi matatizo yetu? Sisi hatuna njia ya kumlisha mtoto. Itoe hiyo mimba mara mmoja!'* Baadaye yeye humpa talaka mumewe. Sehemu nyingine ya ufafanuzi wa thamani ambayo husababisha talaka siku ya leo ni ufafanuzi kuhusu wajibu wa kila mmoja katika ndoa, yaani mume na mke. Ni lazima mume na mke kukubaliana kuhusu jukumu na wajibu wa kila mmoja atakaochukua, na anaotarajia kutoka kwa mwenziwe kabla ya kujihuzisha katika ndoa.

Ni lazima uwe na utangamano wa thamani na yule mtu utakayefunga ndoa naye. Ikiwa nyote mnao umoja ndani ya Kristo, na thamani zenu zimo juu ya Neno lake Mungu, tilia maanani kuhusu utangamano upatikanao hapo! Utangamano wenu wa kiroho utakuwa ndio msingi ambao juu yake, kila mmoja wenu atatumia kuzifafanua nyadhifa na wajibu ambao atatimiza katika uhusiano wenu. Msingi wenu wa kiroho utafafanua mambo ya kitabia na kiroho, na jinsi mtakavyotumia wakati wenu pamoja na fedha zenu, yale yote ambayo nyote mnatarajia kwa watoto wenu na katika kila sehemu ya maisha yenu pamoja.

Historia ya neno utangamano inaanzia wakati watu walipojihisi hivyo kuhusu maisha yao. Utangamano hutokana na shina moja linalomaanisha 'pamoja' na 'kuteseka.' Miaka iliyopita, watu wawili walitambulikana kuwa kamilifu kwa ndoa walipoamua 'kuteseka pamoja.' Hili laonekana kana kwamba ni jambo lisilo jema katika maisha, lakini ndio ukweli. Maisha yalikuwa magumu sana nyakati zile. Je! Umeyatembelea Makanisa ya zamani yaliyo na makaburi na kutambua ni mawe yapi ambayo yalikuwa na alama za kuonyesha kuwa ni makaburi ya watoto? Katika vizazi vya hapo zamani, watu walikuwa kwa kawaida na jamii kubwa. Sababu moja ilikuwa kwamba walifahamu kwamba ikiwa wangelikuwa na watoto kumi, yamkini watano wangeyaepuka mauti.

Utangamano ndiyo moja ya sababu nyingi ambazo ni muhimu sana katika uhusiano wa mawasiliano kati ya mume na mke katika jamii. Ukimpoteza mwanao, mtapitia jaribio hili kwa pamoja. Mtaugua na kuteseka pamoja. Lakini utakapompoteza mwenzio, utateseka peke yako. Nimewahi kuwasikia wengi kati ya washiriki wa ndoa wakithibitisha kweli kwamba wanapokuwa haki pamoja na Bwana na mwenzio, wao huweza kukabiliana na ugumu wo wote. Huu ni ufafanusi mwema wa maelezo sahihi kuhusu maana ya neno 'utangamano.'

Hata hivyo, utumizi wa kawaida wa neno hili umeleta maana iliyopo wakati huu, ambayo ni: 'watu wawili ambao wanaambatana vyema.' Wao wana sifa sawa, tabia, pamoja na thamani na makusudio sawa. Yale watu wanayogundua baada ya ndoa ni kwamba kila mwanadamu ametunukiwa nguvu na udhaifu fulani. Ukweli ni kwamba, wakati mwingi udhaifu haudhihiriki mwanzoni mwa ndoa ile. Ingawa hili halikubaliki, pamoja na ugumu wote uliopo unapodhihirika, wengi wa watu walio katika ndoa siku hizi wanaamua, *'siamini kwamba tuna na utangamano tena, nami nimepata mwingine ambaye ninatangamana naye.'*

Talaka pamoja na kutengana ni mambo ya kawaida siku hizi kwa kuwa jamii inasema kutokuwa na utangamano ni msingi wa kuivunja ndoa. Kweli ni kwamba katika mila na desturi tofauti, unaweza kupata sababu za kila namna za kisheria zinazoruhusu na kurahizisha talaka. Biblia inaruhusu sababu mmoja tu kwa talaka, wala sio kutokuwa na utangamano. Ni uzinifu peke yake. Jinsi ambavyo tayari tumezungumzia hapo awali, agano la ndoa ina sharti moja tu, ambalo ni kutojihusisha na uzinivu. Hali hii inamaanisha kwamba Mungu hahitaji tuishi katika uhusiano huu na mtu mwingine ambaye hawezi kuishi nasi bila ya kutojihusisha na wengine kabisa.

Kukubalika

Ufahamu wetu wa utangamano ni lazima uhusishe dhana ya kukubalika. Yapo mambo mengi sana katika ndoa ambayo ni lazima uyakubali kutoka kwa mwenzio. Yeye hawezi kubadilika. Watu wengi ni wajinga katika mambo mengi; wao hufikiria kwamba wanapofunga ndoa, wataweza kuzibadilisha tabia za wenzi wao ambazo hawapendi. Wanawake ndio wenye hatia ya kuwa na wazo hili. Wao ni wapumbavu hata kufikiria kuwa, *'Baada ya kumuoa yeye, mimi nitamhadaa hadi afanyike kuwa mtu ninayemtaka kuwa.'* Lakini hili ni wazo la kutokomaa. Baada ya ndoa, yule mwanamume atakuwa ndiye mtu aliyemuoa naye hawezi kubadilika.

Maandiko yanawafanyia mzaha watu wale ambao hufikiria kwamba wao wanaweza kujibadilisha wenyewe. Kwa mfano, Yeremia aliuliza, *'Je! Mkushi aweza kuibadili ngozi yake, au chui madoa-doa yake? Kama aweza, ndipo na ninyi mwaweza kutenda mema, ninyi mliozoea kutenda mabaya'* **(Yeremia 13:23).** Biblia inatujulisha kwa njia ya kweli kuhusu kubadilika kwetu.

Lakini, Biblia haituelezi kutimiza matakwa fulani kisha Mungu apate kutubadilisha. Ikiwa wewe kwa hakika umekata shauri kwamba unahitaji kubadilika, au umeshawishika kwamba mwenzio ni lazima abadilike, tumaini lako la pekee la kubadilika huko ni kwako wewe na mwenzio kuzaliwa kwa mara ya pili. Kupitia uzao huu mpya, Mungu anaweza kutubadilisha na kutufanya viumbe vipya ndani na kumpitia Kristo **(2 Wakorintho 5:17).**

Pasipo na tukio hilo la kipekee, watu hawawezi kubadilika. Ni ishara ya kutokomaa kufikiria kwamba unaweza kumbadilisha mwenzio na pia ni ishara ya kutokukomaa kabisa kufikiria kwamba kuwabadilisha wenzi wetu kutasuluhisha matatizo yetu. Utakuja kugundua mapema kwamba umejiunganisha pamoja na kasha lingine la nguvu na unyonge au udhaifu. Ni ishara ya kukomaa kumwuliza Mungu akupe neema ili kuzikubali nguvu na unyonge wa mwenzio katika maisha.

Unapozingatia utangamano wenu wawili katika ndoa, usitilie mkazo juu ya mambo yaliyo kinyume, hasa baadhi ya yale ambayo hayakuzi utangamano. Aina ya yale yaliyo kinyume huangamiza ndoa. Badala yake, tilia mkazo yale yaliyo mema katika utangamano wenu. Kijana mmoja mdogo alizaliwa mara ya pili akiwa na umri miaka kumi na tisa. Wakati alipomweleza mchungaji mwenye busara ambaye alimwongoza kwa Kristo kwamba angekumbana na matatizo katika kuuendeleza usafi wake kutoka kwa zinaa, mchungaji alimpatia mawaidha yaliyokuwa

mema. Alimwambia hivi, *'Mungu anaye mwanamke kwa ajili yako na hili ndilo suluhisho lako kwa upinzani wako na janga la usafi kutokana na zinaa.'*

Huyu mwaminifu mpya akamjibu, *'Je! Mtu atafahamu vipi wakati atakapokutana na yule mwanamke?*' Mchungaji akamjibu, *'Hebu nikueleze wewe. Chukua kipande cha kijikaratasi kisha uchore msitari toka juu hadi chini kwenye kijikaratasi kile. Katika upande wa kushoto wa msitari ule, andika orodha ya tabia zile ambazo ungetaka kuzipata kutoka kwa mwanamke wa kiroho, mwenye akili, mrembo na kadhalika. Baadaye, katika upande wa kulia katika kijikaratasi kile kile, na kando ya tabia na thamani ambazo unataka kutoka kwake utakayemwoa, andika tabia na thamani ambazo huyo mwanamke atahitaji kutoka kwa mwanamume. Tazama orodha ile kwa makini sana halafu ujiulize mwenyewe, 'Je! Mimi ndiye mwanamume yule?' Ikiwa sivyo, basi unafahamu kile unachohitaji kutenda unapoendelea katika maombi na kumgojea yule unayemtarajia na aliyekifikia kiwango chako.'*

Ikiwa wewe umefanya orodha nyingine sawa na ile, utamjua mwenzio utakapokutana naye. Hii ni kwa sababu utafahamu kile unachotafuta. Kwa hakika, kwangu ilitukia hivyo. Mimi niliorodhesha kisha nikaikariri. Wakati nilipokutana na mke wangu, ningelimwambia mahali pale, lakini nilingojea hadi kukutana kwetu kwa mara ya pili ili asinidhanie kwamba nilikuwa mtu asiyesitiri! Ingawa wewe labda haukuwa na orodha hii kwenye mkono wako ulipokutana na mwenzi wako, kwa njia ya kanuni, labda ulikifanya kitu kile kile.

Baada ya kuoana, jiulize mwenyewe, *'Ni thamani zipi kutoka kwa mwenzi wangu zilizonivutia mara ya kwanza na kunifanya kumchangua kama mwenzi wangu katika ndoa yetu?'* Wakati mwingi watu hudumu katika ndoa yao kwa muda hadi pale watakaposahau kitu kilichowavutia kwa wenzi wao. Ni thamani zipi unazozitafuta? Ni ngapi kati ya thamani hizo ambazo bado mwenzio angali nazo?' Sasa ifanye orodha ya thamani zile zote ambazo zina kuvutia kutoka kwa mwenzio, kisha ifanye orodha ya thamani ambazo mwenzio anavutiwa nazo kutoka kwako.

Mchungaji *Dick Woodward* ana jiwe kuu lenye kung'arishwa ambalo lingetumiwa kuwekelea juu ya makaratasi alilopewa kama zawadi na bintiye. Jiwe hili la kuvutia lina swali hili ambalo liliandikwa juu yake: *'Ikiwa wewe hauko karibu kwa Mungu jinsi ulivyo kuwa. . .'* kisha chini ya jiwe hilo kuna maneno haya: *'Ni nani aliye songa?'*

Sasa, liulize swali hilo kuhusu wewe pamoja na mwenzio. Ikiwa haupo karibu jinsi ulivyokuwepo hapo mwanzoni, Ni nani aliyesonga? Je! Ni wewe? Je! Mwenzio ndiye aliyesonga? Usije ukasahau thamani ambazo ziliwavuta pamoja mara ya kwanza.

Maeneo Ya Utangamano

Ili kukusaidia kutazama 'orodha yako ya kale ya utangamano', hebu tutazame baadhi ya mambo ya muhimu ya katika maeneo ya utangamano.

Moja ni utangamano wa kimwili. Katika ndoa nzuri, ikiwa uhusiano wa ngono au wa kimapenzi ni ule ambao Mungu alikusudia kuwa, basi ngono ni asilimia kumi ya uhusiano. Lakini,

ikiwa sio katika mfumo ule ambao Mungu alitayarisha kuwa, ngono inaweza kuwa asilimia tisini ya shida. Hivyo basi, ndoa nyingi huvunjika juu ya kukosa utangamano wa kimwili. Ni kiasi kipi katika kutokuwa na utangamano wako wa kimwili, ikiwa kupo, kungesahihishwa ikiwa ungekuwa mwenye kumjali mwenzio kwanza kabla ya kujijali binafsi, au ikiwa ungemweka mtu mwingine na kutoshelezwa kwake katikati ya uhusiano?

Utangamano pia unahusu thamani. Kamusi inafafanua thamani kama, 'kiwango fulani cha kitu ambacho hukisiwa kwetu kuwa muhimu au kisicho na umuhimu, kilio na matumizi na faida, hivyo kuhitajika kwake.' Kila mmoja wetu ana thamani kama tunaweza au hatuwezi kuzifafanua. Punde tu watu wawili wanapofunga ndoa, hii ni eneo ambayo kutokuwa na utangamano hakika kunaweza kujidhihirisha. Thamani zetu zinasudisha au kudhihirisha mambo mengi, kama jinsi tunavyotumia wakati wetu. Je! Wewe una pingamizi ye yote na mwenzio juu ya jambo hilo?

Thamani zetu husudisha jinsi tutakavyotumia mali au fedha zetu. Fedha na mali zetu ni dhihirisho ya jinsi tunavyoweka hazina zetu. Hivyo basi, wakati tunapotumia fedha zetu, kuna hali tunavyotumia maisha yetu. Je! Wewe pamoja na mwenzio kuna wakati mnapotofautiana kuhusu matumizi ya fedha? Wakati wenzi wanapotofautiana kuhusu jinsi watakavyotumia fedha zao, kuna tabia zinazoibuka ambazo zinaweza kuwa vipimo vyema kuhusu utangamano wao.

Hali nyingine ni jinsi unawapa malezi wanao. Kwa pamoja, ni lazima kujibu maswali haya, 'Ni nini unachotumainia kutoka kwa watoto wetu? Ni elimu ya aina gani tunayotaka kwa watoto wetu? Tunahitajika kuwarudi kwa njia gani watoto wetu?' Kuna uwezekano wa ubishi kati ya mume na mke walio na asili tofauti wakati wanapojibu maswali haya pamoja.

Ufafanuzi wa jukumu la kila mmoja katika ndoa ni jambo muhimu katika utangamano. Maoni yako kuhusu jukumu la mume na baba ni yapi? Je! Maoni yako kuhusu wadhifa wa mke na mama ni yapi? Unapofafanua nyadhifa zenu, ningependa kukuuliza maswali mawili: Je! Mnapata ufafanuzi kutokana na mila na desturi au kutoka katika Maandiko? Ikiwa wewe unaupata ufafanuzi wa wadhifa wako katika mila na desturi, basi je, mambo yanakuendea vipi katika ndoa na jamii yako?

Ikiwa wewe unaamini kwamba Mungu aliumba na kutoa nakala ya ndoa, jinsi unavyofafanua nyadhifa katika uhusiano wako inahitajika kuwa na mizizi yake katika Maandiko. Kumbuka, hoja tuliyoanza masomo haya kwamba ndoa na jamii ni sheria ya maisha ambayo Mungu alianzisha wakati alipomuumba mwanadamu mume na mke. Katika Neno lake, Yeye ametupatia nakala ya jinsi mume na mke pamoja na jamii wanavyoweza kuendelea. Ikiwa unaamini kwamba Biblia ni Neno lake Mungu lililovuviwa, basi unaweza kukaribia Maandiko ukitafuta mpango mtakatifu kwa jukumu hilo. Ikiwa mume na mke wanakubaliana kupata ufafanuzi wa jukumu zao kutoka nakala ya Mungu, hilo litawapa uwezo mkuu katika utangamano wao.

Jukumu Za Kibiblia

Hoja ya kufafanua jukumu za ndoa siku hizi huzoa hoja nyingine ambalo tunaweza kuliita 'hoja kutoka mila na desturi.' Watu watasema kwamba kifungu fulani katika Biblia hakitumiki siku ya leo kwa sababu ya mila na desturi iliyokuwepo wakati Biblia ilipokuwa ikiandikwa. Hoja hii kuhusu mila na desturi inabatilisha kweli ambayo inafundishwa katika Maandiko.

Ni kweli kwamba kuna vifungu vingi ambavyo vinahitajika kutafsiriwa na kufafanuliwa kulingana na mila na desturi, kama **1 Wakorintho 11,** ambapo Paulo anasema kuwa ikiwa mwanamke, kwa kuwa na nywele fupi, yeye anajitangaza kuwa ni kahaba, basi mwanamke Mkristo anapaswa kufanya nywele zake kuwa ndefu. Na ikiwa hakuna mila na desturi sawa na hilo, basi urefu au ufupi wa nywele hautilii shaka.

Lakini vifungu vingi katika Maandiko vina 'desturi na mila ambazo zakubalika kote ulimwenguni,' kumaanisha kwamba havihitaji kutafsiriwa au kufafanuliwa kulingana na mila au desturi vilivyoandikwa. Tunahitajika kutafsiri mila na desturi zetu kuambatana na Maandiko. Haturuhusiwi kutafsiri Maandiko kuambatana na mila au desturi. Maandiko yalitolewa hili kuanzisha na kuimarisha desturi na mila za Kiungu. Fungu moja liko katika kitabu cha Mwanzo pale Mungu alipomuumba mwanamke kuwa msaidizi, au mkamilishaji wa mwanamume. Mwanamume alikuwa si mkamilifu bila mwanamke. Mwanamke naye alikuwa ni mpungufu bila mwanamume. Mwanamume na mwanamke wakiunganishwa pamoja wanaitwa 'Adamu.' (wala sio 'bwana na bibi Adamu').

Bila mke, mwanaume ni sehemu moja ya kile anachohitajika kuwa. Bila mwanamume, kwa hakika mwanamke amepungukiwa. Lakini Mungu huwaleta hawa wawili pamoja nao hufanyika mtu mmoja mkamilifu. Hii ni jumla ya maelezo ya desturi na mila nyingi (hili halibatilishwi na mila au desturi ye yote ile), za Kibiblia.

Mfano Wa Ndoa Ya Petro

Kifungu kingine cha Maandiko chenye 'desturi na mila zinazokubalika kote ulimwenguni' kinapatikana katika sura ya tatu ya waraka wa kwanza wa Petro. Katika sura iliyotangulia, Petro alinukuu kweli kwamba, kabla yetu kufanyika waaminifu, tulikuwa kama kondoo waliopotea. *'Lakini sasa mmemrudia Mchungaji na Mwangalizi wa roho zenu'* **(2:25).**

Kisha anaanza sura ya 3 kwa mashauri kwa wanawake walio na waume ambao hawalitii Neno lake Mungu. Yeye anaandika haya: *'Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu, kusudi, ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno*' **(3:1).** K*wa waume aliandika hivi: 'Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe'* **(3:7).**

Msemo mkuu katika mstari wa 1 na 7 ni 'kadhalika.' Vipi? Petro anaelezea maneno hayo, 'Mchungaji na Mwangalizi wa roho zenu.' Katika Maandiko yao, Petro na Paulo wanauonyesha mfano wa waume na wake. Mfano huo ni Kristo na Kanisa.

Petro anaonyesha Kanisa na Kristo na anauliza waume na wake, 'Je! Mnataka kuona 'desturi na mila za Mungu zinazokubalika kote ulimwenguni' za jukumu zao? Kisha tazama jinsi Kristo anavyolichunga Kanisa lake. Waume, wachungeni wake zenu, jinsi Kristo anavyolichunga Kanisa lake. Je! ungependa kufahamu wajibu wako kama mke? Basi, utazame mfano huu wa Kristo na Kanisa. Mume wako akizidi kukuchunga, kama alivyo Kristo kwako, kuwa jinsi Kanisa lilivyo kwa Kristo katika uhusiano wako na mumeo.'

Hii ndio roho ambayo Petro anakiandika kifungu hiki. Yeye kwa hakika anaandika hivi: 'Wake, waacheni waume zenu wawe jinsi Kristo alivyo kwenu. Waacheni wawachunge ninyi. Waacheni wawapende ninyi jinsi Kristo alivyoipenda Kanisa.' Hivi ndivyo inavyomaanisha kusadiki kwa wake-kuwapa nafasi waume zao kuwachunga jinsi Kristo anavyolichunga Kanisa.

Sababu ambayo hatushuhudii mfano au kielelezo hiki katika ndoa nyingi za waaminifu siku ya leo sio kwamba wake hawajitolei kwa uchungaji wa waume zao, ingawa hiyo ni moja ya shida zilizopo. Kizingiti kikuu kwa mfano huu wa ndoa hii kutimilizwa na kudhihirika siku ya leo ni kwamba waume hawako kama Kristo alivyo kwa wake zao. Wao hawafanyiki makuhani wa nyumba. Wao hawauchukui wajibu wao katika kuongoza na kuwachunga wake pamoja na jamii zao.

Mfano Wa Ndoa Ya Paulo

Katika sura ya tano ya waraka kwa Waefeso, Paulo anafafanua nyadhifa za waume na wake ambazo zinalingana na zile zilizo katika nalaka ya Petro. Paulo anaadika katika mstari wa 21: *'..hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo.'* Tambua kwamba Paulo anahimiza kunyenyekeana kwa yule mwingine. Waume na wake ni lazima wanyenyekeane kila moja kwa yule mwingine kwa kuwa ni asili yao kujipenda wenyewe. Wakati wenzi waaminifu wanaposoma kwamba wawili wanahitajika kuwa mmoja, wao huishi kwa miaka mingi wakiulizana, 'Ni yupi?' Hili wawili kuwa mmoja, kuifanya ndoa kunawiri, wote yaani mke na mume ni lazima wanyenyekee yule mwingine. Hii ndio maana ya upendo.

Paulo anaendelea kusema, *'Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo'* **(22-24).**

Ni dhahiri kwamba Paulo anatenda jambo ambalo Petro alilitenda katika mashauri yake ya ndoa. Petro na Paulo wanainua juu mfano wa Kristo na Kanisa na wote wanaandika fafanuzi zao za wajibu wa wake na waume wakitumia Kristo na Kanisa kama mfano wao. Mfano huu wa Kristo na Kanisa haukuhusika kwa lo lote la mila za Asia Ndogo au Roma. Nakala hizi za ndoa zilibadilisha mila na desturi zilizozorota na zenye uharibifu katika siku zao. Ni lazima tukumbuke kwamba Yesu hakuwafunza wanafunzi na mitume wake kuzikaribisha thamani zilizokuwepo katika mila na desturi zao. Yeye aliwapa changa moto kubadilisha mila na desturi zao.

Sasa, kazi waliyopewa wanawake katika mashauri ya Paulo kuhusu ndoa inahitaji neema ya Mungu. Ingawa kazi ya wanaume inahitaji neema zaidi ya Mungu. *'Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake'* **(25).** Kwa njia ile ile

ambayo Kristo alilipenda Kanisa, waume wanahitajika kuwapenda wake na jamii zao. Jinsi Kristo alivyojitolea kwa Kanisa, waume wanahimizwa kujitolea wenyewe kwa wake na jamii zao. Yesu aliwaamuru waume *'Kuwa wakamilifu jinsi Mungu alivyo mkamilifu'* **(Mathayo 5:48).** Paulo aliwaandikia Wakolosai kwamba tumaini letu la pekee ni miujiza kwamba Kristo anaishi ndani yetu. Ikiwa Kristo anaishi ndani yetu, inawezekana - hata kawaida - kwetu kuwa kama Kristo alivyo, tunapojitolea na kuwapenda wake zetu **(Wakolosai 1:27).**

Mwanamke, ikiwa una mume anayekupenda na watoto wako jinsi Kristo alivyoipenda Kanisa, je lingekuwa vigumu kumruhusu kukuchunga? Ingekuwa vigumu sana kumruhusu kuwa kichwa cha nyumba na kutwaa wajibu wa kuiongoza nyumba yako?

Katika hali sawa na hilo, wanawake huepa kwa urahisi sana. Petro kwa hakika anawaandikia wake, *'Waacheni waume kuwachunga ninyi, na kufurahia.'* Hili ndilo Petro analolimaanisha wakati anapoandika, *'Ili kwamba wakapate kuvutiwa. . . kwa tabia za wake zao. Roho ya upole na yenye utulivu ni ya thamani kuu machoni pa Mungu.'* Furahia katika kujinyenyekea kwa mume wako. Wanawake wengi hujitolea kwa uso tu ilhali kwa ndani ni waasi. Lakini Petro anaandika, 'La hasha! Kujitolea kwenu na kuwe kwa kweli; na kutoke ndani mwenu. Furahia kuhusu kujitolea huko. Na uwe kimya. Na kwa urahisi, fanyika kuwa Neno mbele ya mumeo. Ikiwa kutakuwepo na kitu cha kumpa changa moto kusimama na kutwaa wadhifa wake, ni wewe kusimama katika wajibu wako.'

Kumbuka kwamba Petro anatangaza maneno haya kwa wake ambao waume zao hawalitii Neno. Haya yanaweza kumaanisha kwamba hawa waume sio waaminifu. Pia inaweza kumaanisha kwamba waume zao ni waaminifu lakini hawawi kwa wake zao jinsi Kristo alivyo kwa Kanisa. Kuna mahali ambapo mume na mke wanahitajika kusimama katika ndoa kulingana na Yesu, Petro na Paulo. Tunahitaji kukumbuka kwamba Petro ananena maneno haya kwa wake ambao waume zao hawasimami mahali wanapokusudiwa.

Kwa Mhutasari

Muhimu, Petro anawaambia wake hawa kwamba wasiwasukume waume zao mahali wanapokusudiwa kuwa, au kuwahubiria hadi pahali hapo, wala kuwavuta hadi pahali pale. Kwa neema ya Mungu, wao wanahitaji kusimama mahali pao. Yeye hawaambii kwamba mashauri yake yatawaongoza waume zao hadi katika wokovu au kubadilika kwa tabia zao. Mashauri yake ni kwamba, ikiwa kuna lo lote ambalo litasuluhisha shida yao; itakuwa ni mfano walio kwa waume zao ambao unaweza kuwapa changa moto kusimama mahali wanapohitajika kuwa.

Sura ya 6

Kiunganisho Cha Upendo

Hali ya kiroho ndio msingi wa umoja ambao Mungu alifanya kwa mume na mke. Mawasiliano ni chombo ambacho wenzi wanaweza kupalilia na kuendeleza umoja wao. Utangamano ni ishara ya umoja huo wao. Upendo ni nguvu kuu ya umoja ambao Mungu aliunda wakati alipotangaza kwamba wawili ni mwili mmoja.

Hili ni swali nzuri la wenzi wawili kujiuliza kabla ya kuingia katika ndoa: ‘Unapomwambia mwenzio kwamba, ‘Ninakupenda,’ huwa unamaanisha nini? Je! Unamaanisha kwamba, ‘Nina haja hili nawe unalitimiza vyema kuliko ye yote niliyewahi kukutana naye?’ Wakati unaposema, ‘Nina kupenda,’ je! Kwa hakika unasema, ‘Nikuhitaji wewe?’ Ikiwa hii ndio tafsiri yako ya dhana kuhusu upendo, basi hauna mtazamo wa Kibiblia kuhusu maana ya neno ‘Upendo.’

Unaposema, ‘Ninakupenda,’ je! Unamaanisha, ‘Nafsi yako ni muhimu sana kwangu jinsi nafsi yangu ilivyo?’ Hili ni bora, lakini halifafanui upendo wa Kibiblia, upendo wa Mkristo.

Shida kuu iliyo katika ndoa nyingi ni kujipenda mwenyewe au uchoyo. Vivyo hivyo, kasi kuu katika ndoa ni kutojipendelea na kuwajali wengine au uwezo wa kuyapa mahitaji ya wale wengine kipao mbele. Unapotambua ufafanuzi ya Biblia kuhusu upendo, utaona kwamba upendo unaofafana na ule wa Kristo ndio uwezo mkuu katika ndoa kwa kuwa upendo wa Kristo unatuwezesha kutojitakia wenyewe.

Yesu alisema, *‘Ni baraka zaidi kupeana kuliko kupokea’* **(Matendo 20:35).** Ndoa zinaweza kubadilishwa wakati funzo hilo moja la Kristo linapotimizwa. Wakati watu wengi wanapofunga ndoa, wao huwa tu wapokeaji. Hujaribu kuchukua kutoka kwa wenzio ili kutimiza mahitaji yao. Ikiwa wote wawili ni wapokeaji na hakuna mmoja anayetoa, basi hakuna mmoja anayepokea cho chote. Lakini, vipi mambo hubadilika wanapotambua kwamba ni kutoa kuliko kupokea!

Ikiwa haujajifunza kuwa mtu mwenye kujali sana wale wengine, tafadhali usizae watoto. Kama ilivyo kujitolea katika ndoa, wenzi waaminifu hawapaswi kuzaa watoto hadi wakati Bwana atakapowaongoza kwa hali hiyo katika ndoa. Kuwepo na watoto ndio jambo la kutokujipenda ambalo wenzi wanaweza kutenda. Zaidi ya miaka ishirini hadi ishirini na mitano ya malezi ya watoto wao, ni lazima watoe na kutoa bila kutarajia kupokea cho chote. Ikiwa ni wazazi wema, watoto wanahama nyumbani mwao, na kufunga ndoa kisha kuzaa watoto wao. Hii ni hoja ambayo inahitaji kutojipenda mwenyewe.

Labda mimi ni mmoja wa kizazi kinachotoweka siku za leo. Mimi nilijaliwa kuwa na mama aliyekuwa anataua na kuamini ya mfano wa Mungu kuhusu ndoa na jamii. Mama mzazi wangu alikuwa na watoto kumi na mmoja. Siku moja nilipata kumwuliza hivi, ‘Ikiwa ungepata fursa nyingine na kuanza upya maisha haya, ungetuzaa wote?’ Yeye alinijibu, ‘Ndio, ningefanya hivyo, lakini kabla ya kutenda hivyo, ningekuwa nimeazimia kwamba singeishi maisha yangu peke yangu.’ Labda yanasikika tofauti kwako kwamba mamangu angechangua ‘kutokuwa na maisha yasiyo yake mwenyewe.’

Mojawapo ya hakika za kijana wa karne hii ya ishirini na moja ni haki ya ‘kuwa na maisha yake mwenyewe’ na kuishi maisha yale. Hii ndiyo sababu wanawake wengi hukwazwa na wazo kwamba wanahitajika kuwakamilisha waume. Waume pia hukwazwa kwa wazo kwamba wanahitajika kuwapenda na kujitolea kwa wake zao jinsi Kristo alivyoipenda na kujitolea mwenyewe kwa Kanisa. Je! Unawezaji kupokea maisha na kuishi kwa ajili yako binafsi na bado ujitolee mwenyewe kwa mkeo na jamii? Jibu ni kwamba haiwezekani.

Lilisemekana kwake Kristo kuwa *'Yeye aliwaokoa wengine, lakini hangelijiokoa Mwenyewe'* **(Mathayo 27:42).** Ili kupenda na pendo lake Kristo, ni lazima utoe maisha yako dhabihu kwa wale unaowapenda. Mama yangu alimpenda mume na watoto wake kwa pendo lake Kristo. Hii ndio sababu hakuwa na maisha yake ya kibinafsi. Lakini alikuwa mwenye furaha! Yeye alikuwa na ndoa ya miaka mingi, na hakuna siku moja alisoma kitabu kuhusu ndoa. Yeye alisoma Biblia peke yake. Alikuwa mke na mama mwenye furaha kwa sababu alipata nguvu na kasi ya ndoa kutoka kwa Biblia yake.

'Aina ya upendo' aliouchagua kuishi ni kinyume cha hali ya kizazi cha 'mimi pekee.' Vivyo hivyo, usemi huu wa Yesu: *'Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake'* **(Yohana 15:13).** Au fundisho hili la Yesu: *mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza*.' **(Luka 9:24).** Mmishionari mmoja aliyeuawa kwa ajili ya imani yake aliandika hivi: *'Yeye si mjinga ambaye anapeana kile ambacho hawezi kukihifadhi kwa ajili ya kile ambacho hawezi kukipoteza.'* Uamuzi wa kusalimisha maisha yako kama dhabihu kwa niaba ya mtu au watu wengine, ndiyo upendo mkuu. Hii ndio namna au aina ya upendo ambao unaonekana katika fafanuzi ya wajibu wa mume na amke ambao wameunganishwa pamoja katika ndoa ambayo iko katika Biblia.

Thamani ya upendo wa aina hii ni kasi au uwezo wa umoja. Kwa muhtasari: Uhusiano wa kiroho ambao wenzi walio na Kristo binafsi au pamoja, ni msingi wa umoja; nao mawasiliano ni chombo ambacho hudumisha umoja huo; utangamano ni ishara ya umoja huo, na upendo ndio nguvu na kasi ambayo inaendesha umoja huo.

Hivyo Basi, Upendo Ni Nini?

'Je! Unamanisha nini unapomwambia, 'Ninakupenda?' Jinsi nimewauliza waume swali hili, nimeshangazwa na jinsi wao hutatanika kwa kulitafuta jibu halali kwa swali hilo, au kufafanua kile wanachofikiria kuwa ndio upendo. Ukweli ni kwamba, tunapofanya ndoa tungali wachanga, inawezekana kwamba hatufahamu lo lote kuhusu upendo. Wakati kijana anapomwambia msichana anayevutiwa naye, 'Ninakupenda,' kile labda huwa anamaanisha ni kwamba, 'ninakupenda na ninakutaka wewe.' Ikiwa hili ndilo mwanamume analomaanisha wakati anapomwambia bibi harusi wake kwamba anampenda, basi humwacha mkewe bila usalama kwa kuwa baadaye, yule mumewe anaweza kumpata mwingine ambaye anaweza kutimiza mahitaji yake zaidi kuliko mkewe.

Sura Ya Upendo Ya Biblia

Hebu nishiriki nanyi kile ninachoamini kuwa ndio ujumbe mkuu kuwahi kuandikwa kuhusu upendo wa Mungu na Kristo. Umenakiliwa katika sura ya kumi na tatu ya Wakorintho wa kwanza. Upendo haukuwa somo kuu alilokuwa akilizungumzia wakati alipoandika kitabu hiki cha Wakorintho. Kwa hakika, yeye alikuwa akiandika kuhusu vipawa au karama za kiroho, na ni katika kuelezea vipawa hivyo alipoliandika sura hii kuhusu upendo.

Upendo Walinganishwa (1-3)

'Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidi kitu' **(1-3).**

Katika mistari ya kwanza mitatu ya sura hii kuu, Paulo anaandika kwamba upendo haulinganishwi wala kubadilishwa na cho chote. Kwa hakika, anaandika, *'Mimi si kitu, sina cho chote kile, hamna kile niwezacho kukitenda, na cho chote kile nitakachokuwa, nilicho nacho, au kukitenda kinaweza kuichukua nafasi ya upendo katika maisha yangu.'* Katika siku zake Paulo, wale walioishi katika mila na desturi ya Kiyunani (Griki) na Korintho walifahamika sana kwa ufasaha wa kunena na kutilia mkazo elimu, hasa filisofia. Waaminifu katika Kanisa la Koritho wastahi sana karama za kiroho, na zaidi karama ya kunena kwa lugha. Hii ndio sababu Paulo analinganisha kupenda ufasaha wa usemi, lugha za malaika, na kuwa na elimu yote, kuweka mbele umuhimu wa kutolinganishwa na kutobadilishwa kwa upendo ambao anaandika kuhusu.

Paulo baadaye anataja karama ya unabii, ambayo ataitaja kama karama kuu zaidi ya karama nyingine **(1 Wakorintho 14:1).** Yeye pia analinganisha upendo na imani na kujumuisha sura hii akituambia kwamba imani ni mojawapo ya thamani tatu za uzima wa milele. Kama mmishionari mkuu Kanisa kuwahi kupata, pia tunambua jinsi imani ilivyokuwa muhimu kwake Paulo. Hata hivyo, aliandika kwamba ikiwa tutakuwa na imani bila upendo, sisi si kitu. Paulo anapolinganisha upendo na thamani ambazo Wakoritho wanatambua kuwa muhimu, yeye anamalizia kwa kusema: 'Hamna cho chote kati ya hizi ambacho kinaweza kubadilishwa katika maisha yako, kwa upendo.'

Upendo Watofautishwa (8-13)

'Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. Kwa maana tunafahamu kwa sehemu; na tunafanya unabii kwa sehemu; lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika. Nilipokuwa mtoto mchanga, nalisema kama mtoto mchanga; nalifahamu kama mtoto mchanga, nalifikiri kama mtoto mchanga; tokea hapo nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto. Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana. Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo' ***(8-13).***

Mwishoni mwa sura hii, Paulo anamalizia kulinganisha upendo wakati anaposhiriki nasi kwamba kuna vitu vitatu ambavyo ni thamani za milele: tumaini, imani na upendo. Lakini, anamalizia kwa kusema kwamba kilicho kikuu katika thamani hizi za milele ni upendo. Tumaini ni thamani yenye kudumu kwa kuwa huongoza katika imani. Siku moja tumaini letu, au kusadiki kuna kitu fulani chema katika maisha haya, na hupata uhakika wakati kunapotuongoza kwa imani **(Waebrania 11:1).** Imani ni mojawapo ya thamani zinazodumu kwa kuwa hutuongoza kwa Mungu. Lakini, wakati tunapogundua upendo, hatugundui kitu kinachotuongoza kwa kitu kingine, bali kwa Mungu. Tumemgundua Mungu, kwa kuwa tuna thamani katika upendo ambao ni sehemu ya Mungu. Hii ndiyo sababu upendo hauwezi kubadilishwa wala kulinganishwa na cho chote **(1 Yohana 4:16).**

Furushi La Upendo (4-7)

'Upendo huvumilia, hufadhili, upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote' **(4-7).**

Katika kitabu chake cha injili, Kitu Kikuu katika Ulimwengu, *Henry Drummond* aliandika kuhusu misitari ya 4 hadi ya 7, 'Katika mistari hii, Roho Mtakatifu anaipitisha dhana ya upendo wa Kiungu katika kiio cha maarifa ya Paulo yaliyovuviwa, na kutokea upande ule mwingine kama furushi la thamani.' Sifa kumi na tano zinatiliwa mkazo katika mistari minne ya Wakorintho wa kwanza. Ukikagua sifa hizi, utajipata mwenyewe ukikagua eneo kubwa la upendo wa Kiungu na maelezo ya asili ya Mungu kwa kuwa tumeambiwa kwamba Mungu ni Upendo **(1 Yohana 4:16).**

Ni vigumu sana kuelezea Mungu au upendo ambao ni Mungu. Kwa hekima kuu, na uvuvio wa Roho Mtakatifu, Paulo anatueleza jinsi upendo wa Kiungu ulivyo. Kwa hakika, yeye anasema hivi, 'Ikiwa una upendo huu ambao ninaandika juu yake, hivi ndivyo utajikuta ukiwatendea watu ambao hukutana nawe maishani.' Katika waraka mwingine wenye uvuvio, Paulo anatuambia kwamba tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili na uaminifu' **(Wagalatia 5:22).** Kwenye mistari hii minne katikati mwa sura ya upendo, Paulo anaweka upendo huo kwenye darubini.

Ningependa kukupa changa moto kutenda jambo fulani. Kwa uangalifu, chunguza sifa hizi kumi na tano ambazo zinaelezea kuhusu upendo mkuu. Unapofanya hivyo, weka mwenzio, watoto wako, na watu wengine katikati mwa kila thamani ambayo inaeleza kuhusu tunda la Roho Mtakatifu likitoka katika maisha yako. Watu wana uwezo wakupindua kifungu hiki na kufikiri kuwa, *'Sasa, hivi ndivyo mwenzi wangu na waaminifu wengine wanavyopaswa kunipenda.'* La! Hasha! Hivi ndivyo Paulo anavyosema, *'Unahitajika kumpenda mwenzio na watu wengine.'*

Wakati mtoto anapokuwa na umri wa miaka miwili, mtazame kwa makini akienda shule ya watoto wachanga. Utapigwa na butwaa wakati atakapochukua kipuzi cha kuchezea kutoka kwa mwingine na kusema, *'Yesu alisema twahitajika kushiriki!'* Kwa hakika, huwa ajajifunza maana kweli ya upendo ambao Paulo anautambulisha kwetu katika sura hii. Sisi watu wazima tuna hila kuhusu jambo hili, ingawa kwa kweli tunalitenda. Tunaposoma kifungu hiki kuhusu upendo, wengi wetu hufikiria, *'Hivi ndivyo mwenzi wangu anavyohitajika kunipenda!'* Unapozidi kutazama thamani hizi ambazo zinadhihirisha upendo wenye uvuvio, usifikirie kuhusu mwenzio anavyostahili kukupenda. Jiulize mwenyewe, ' *Je! Mimi ninampenda mwenzi wangu kwa njia hii?'* Sasa hebu tutazame thamani hizi moja kwa moja:

Upendo 'hauna kivuli.' Neno la Kiyunani ambalo ni sawa na lile Paulo alilotumia linamaanisha 'ukarimu.' Hili linasimulia hali ya kutojipendelea au kuwa mchoyo kwa watu wale wengine. Uje, wewe umejitolea kwa haki kuwa bila uchoyo utatoa muda wako, nguvu na cho chote ulicho nacho kwa haja na mahitaji ya mwenzio? Hilo ndio tafsiri ya 'kutokuwa na kivuli'.

Upendo ‘hauna wivu.’ Hili ni tafsiri ya Kiyunani ambalo linamaanisha kuwa mtu aliye na upendo wa iana hii hajisifu. Yeye hana haja ya kujionyesha kwa watu wale wengine. Hatakuwa na wazo kuu juu ya umuhimu wake kwa sababu upendo huu unamfanya kuwa mnyenyekevu. Hili litakuwa kinyume cha kiburi na ufidhuli wa dunia hii.

Maeneo Mawili Ya Upendo Tukufu

Sifa hizo zote za utu zina maeneo ya utu wa nje na wa ndani. Kwa nje, upendo uko hivyo kwa hakika ya utu wa ndani ambao unadhihirisha upendo. Tunaona hili katika msitari wa 5: *‘Upendo haukosi adabu.’* Kwa nje, upendo hauna tabia mbovu. Tabia yake ni upole, heshima, kwa kuwa haijitakii mambo yake mwenyewe.’ Shukrani kwa kweli hii ya ndani, *upendo huu haukasirishwi kwa haraka **(5)***. Hauna hasira nyepesi, wala hauchokozeki kwa kuwa hauendelezi matakwa yake mwenyewe au kulazimisha matakwa yake mwenyewe. Ni vigumu sana kumkasirisha mtu ambaye anapenda na huwajali watu wengine zaidi. Hii ndiyo dhihirisho la nje la kweli iliyomo ndani ambayo haigandamizwi na kujitakia makuu, majivuno, na tabia inayosema ni kulingana na njia yangu au sivyo.

Upendo ‘haufikirii mabaya.’ Hii ni tafsiri ya neno ambalo Paulo alitumia na maana yake ni kuwa upendo hauhesabu mabaya, au kwamba upendo hutimiza lengo lake. Je! Wewe unamhesabia mabaya mwenzio? Ikiwa unatenda hivyo, hilo halitokani na upendo wake Kristo aliye moyoni mwako. Sababu kutolitenda hili ni kuwa, ndani yake haliweki hesabu kwani ‘haifurahii maovu.’ Hii inamaanisha kwamba mtu anayependa kwa upendo wake Kristo hapendezwi wakati chombo cha upendo huo kinapoanguka. Ikiwa chombo cha upendo kimeshidwa, mpenzi huadhirika. Yeye hataki chombo cha upendo kuanguka. Ndani yake hupendezwa wakati chombo cha upendo kinapofanikiwa. Hii ndiyo maana ya ‘kufurahia katika kweli.’ Kupendezwa wakati kweli inapofanikiwa katika upendo na chombo cha maisha ni dhihirisho la upendo wake Kristo.

Msitari wa 7 unatuambia kwamba upendo *‘huvumilia yote, huamini yote, hutumainia yote, na hustahimili yote.’* Wakati chombo cha upendo kinapoanguka, mpenzi hukaa kimya. Hii ndio maana ya ‘kuvumilia mambo yote.’ Upendo una imani ya kuona na kuamini katika uwezo wa chombo chake.

Wakati nilipokuwa kijana na uwezo wangu mdogo kuonekana, mchungaji wangu alinitendea hili na lilikuwa jambo la maana sana kwangu. Alikuwa akisema mara kwa mara, *‘Mimi nina imani nawe kwa lile litakalotukia hapo baadaye.’* Kwa wakati ule, mimi sikufahamu mtu mwingine aliyekuwa na imani kwangu. Hili lilikuwa jambo kuu kwangu. Hapo mwanzoni, nilifikiria kwamba huu ulikuwa mzaha tu, lakini yeye haikuwa hivyo. Kwa hakika, yeye alikuwa na imani kuu kwangu. Aliamini mambo yote.

Kwa sababu upendo una imani ya kuona uwezekano ndani mwa mwingine, hutumainia yote, kumaanisha kwamba hungojea kwa furaha utimizo wa yale ambayo huyaona na kuamini. Kisha huku ukiendelea kuamini na kungojea utimilifu wake, huyavumilia yote. Neno la Kiyunani lililotumiwa katika nakala ya mwanzo linamaanisha ‘kuvumilia hali kwa kuamini na kungojea.’ Haya yote yanadhihirishwa kwa nje kwa kuwa ndani, mpenzi ana ujasiri huu uliotakaswa. Ujasiri wao hauko katika chombo cha upendo.

Mwishowe, Paulo anatuhakikishia kwamba ‘upendo haupungui.’ Sisi hupungukiwa katika kupenda, lakini upendo haupunguki. Yule anayependa anafahamu kwamba upendo ambao yeye huwapenda hautapunguka au kubatilika na kugusa chombo cha upendo. Kwa maelezo mengine, mpenzi anaweza kusema kwa mpendwa wake, ‘hakuna lo lote usemalo au kutenda linaloweza kunizuhia kukupenda, kwa sababu mimi ninakupenda kwa pendo lake Kristo ambalo ni thabiti. Huyavumilia mambo yote.’

Katika sifa hizi kumi na tano, mtazame mwenzi wako na kujiuliza, ‘Wakati ninaposema kwamba ninampenda, huwa ni namaanisha nini?’ Ikiwa Roho Mtakatifu yumo ndani yako, wewe una uwezo wa kumpenda mwenzio. Huu ndio uwezo ambao Mungu ameunda ili kuendeleza umoja kati ya watu wawili ambao wako katika ndoa. Bila uwezo huu, umoja wenu ni kipande cha Roho ya sheria ya ndoa na jamii. Lakini, kwa neema yake Mungu, wewe unafahamu kwamba upendo unaweza kufanya umoja wenu kuwa kila kitu ambacho Mungu alikusudia kuwa.